# Nipashe

Jumatano Januari 29, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580140

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US




## Mahakama yasitisha kesi Bilionea Msuya familia zifikie maridhiano

UKURASA 3



Miaka 75 kukombolewa kambi ya mateso Poland

siasa

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU

Kinamama Shinyanga wachechemea serikali mitaa, wapania uchaguzi mkuu

NEC inavyoshika kasi kudodosa kona zote kuboresha daftari kura

• Machi kuanika ilichofanya mikoa 31

Bunge Marekani linavyokerwa na mipango ya Rais wao Trump

UKURASA 13

# TMA yahadharisha mvua kubwa nchini

• **Yatabiriwa** kunyesha kwa siku tano mfululizo, mikoa husika yawekwa bayana... *Endelea ukurasa 2*


## YALIYOMO

UKURASA WA 8

**WASHTAKIWA MAUAJI YA MVUNGI WAMKATAA HAKIMU**

WASHTAKIWA wanaokabiliwa na kesi ya mauaji ya aliyekuwa Mjumbe wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba...

UKURASA WA 9

**DC AMSWEKA NDANI MKUU WA CHUO TUHUMA NZITO**

MKUU wa Wilaya ya Kilolo mkoani Iringa, Asia Abdallah, amemweka ndani Mkurugenzi wa Chuo cha Maendeleo...

UKURASA WA 24

**DIWANI MATATANI KWA TUHUMA KUTISHIA KUUA**

DIWANI wa Kata ya Kining'inila (CCM) Halmashauri ya Wilaya ya Igunga mkoani Tabora, Elisha Anthony...




Mkazi wa Jiji la Dar es Salaam, akiangalia mabaki ya gari lililoteketea kwa moto na kutelekezwa takribani siku ya pili sasa bila ya kuondolewa na kusababisha usumbufu wa foleni za magari katika Barabara ya Mwai Kibaki, eneo la Kawe, jijini jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Wadaiwa sugu NHC wawekwa tumbo joto

UKURASA 3

## Bulaya ataja mambo matano unadhimu kambi ya upinzani

UK.2




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store



**MICHEZO** **KABWILI AWASHA MOTO SIMBA, TFF** UK.31

**MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

# Hali ya hewa yahadharisha mvua kubwa

Na Mwandishi Wetu

MAMLAKA ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) imetoa tahadhari kwa wananchi wanaoishi katika mikoa ya Kanda ya Ziwa, Kaskazini na Kanda ya Kati kukumbwa na mvua kubwa kwa siku tano mfululizo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na mamlaka hiyo, mvua hizo zinatarajia kunyesha katika mikoa ya Mwanza, Simiyu, Shinyanga, Mara, Kagera, Geita na Tabora kwa Kanda ya Ziwa.

Mikoa ya Kanda ya Kati itakayokumbwa na mvua hizo ni Singida na Dodoma huku mikoa ya Kanda ya Kaskazini ikiwa Kilimanjaro, Arusha na Manyara.

Sambamba na mikoa hiyo, taarifa hiyo ilisema mikoa ya



Nyanda za Juu Kusini ambayo ni Rukwa, Iringa, Mbeya na Njombe pia itakumbwa na mvua hiyo.

Aidha, taarifa hiyo ilieleza kuwa mvua hizo zinatarajia kusababisha uharibifu wa miundombinu na mali kwa baadhi ya maeneo pamoja na makazi kuzungukwa na maji.

"Athari zinazoweza kujitokeza kutokana na mvua hizo ni baadhi ya makazi kuzungukwa na maji, ucheleweshwaji wa usafiri na kusimama kwa muda kwa baadhi ya shughuli za kiuchumi na kijamii," ilisema taarifa hiyo.

Kutokana na hatari hiyo, TMA imewatahadharisha wananchi wanaoishi katika mikoa hiyo, kuchukua tahadhari mapema pamoja na kujiandaa.

Mvua kubwa nchini zilianza kunyesha Desemba, mwaka jana katika mikoa mbalimbali na kusababisha maafa ikiwamo vifo, mafuriko na uharibifu wa miundombinu.

Katika mkoa wa Lindi, kwa mfano, zaidi ya watu 600 walizama katika mafuriko, hivyo jitihada kubwa kufanyika na hatimaye kuwaokoa.

NHC
SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA
TUNAJENGA TAIFA LETU

TAARIFA KWA UMMA

Shirika la Nyumba la Taifa linapenda kuwatangazia wapangaji wake wote wenye malimbikizo na waliohama na madeni wakiwamo watu binafsi, taasisi za umma, wakala za serikali na kampuni binafsi kulipa malimbikizo na madeni hayo katika kipindi cha siku 14 kuanzia tarehe ya tangazo hili na watakaoshindwa kufanya hivyo katika muda uliopangwa hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao. Shirika litawatangaza wadaiwa SUGU wote kwenye vyombo vya habari.

Kwa wale wanaofahamu kwamba upangaji wao ulipatikana kwa njia zisizo sahihi wanapaswa kutoa taarifa Makao Makuu ya Shirika ili kuweza kurasimishwa.

*Epuka usumbufu lipa kodi kwa wakati.*

Imetolewa na:

OFISI YA MAWASILIANO KWA UMMA NA HUDUMA KWA JAMII
NHC- MAKAO MAKUU



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na Spika wa Bunge Job Ndugai (wa pili kulia waliokaa), wakiwa na maspika na mawaziri wakuu wastaafu katika hafla ya kukabidhi majoho kwa maspika wastaafu jijini Dodoma, jana. Waliokaa (kutoka kushoto) ni Mbunge wa Urambo, Margaret Sitta ambaye ni Mke wa Spika mstaafu, Marehemu Samuel Sitta; Spika mstaafu, Pius Msekwa na kulia ni Spika mstaafu, Anne Makinda. Waliosimama ni mawaziri wakuu wastaafu. Kushoto ni Frederick Sumaye, Edward Lowassa na John Malecela. **PICHA: OWM**

# Bulaya ataja mambo matano mnadhimu kambi ya upinzani

Na Godfrey Mushi, DODOMA

MBUNGE wa Bunda Mjini (Chadema), Ester Bulaya, ameteuliwa kuwa Mnadhimu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, huku akitaja mambo matano atakayoyasimamia kwa miezi sita iliyobaki, kabla ya Bunge kuvunjwa kuelekea uchaguzi mkuu utakaofanyika Oktoba, mwaka huu.

Bulaya alitangazwa jana bungeni jijini Dodoma na Spika wa Bunge, Job Ndugai kurithi mikoba ya Mbunge wa zamani wa Singida Mashariki, Tundu Lissu.

"Mheshimiwa Freeman Mbowe ameniandikia kunijulisha kwamba Mnadhimu Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni atakuwa Mheshimiwa Esther Bulaya. Karibu sana Mheshimiwa Esther ufanye kazi karibu na Mheshimiwa Jenista Mhagama pale ili mambo yetu yaweze kwenda," alisema Ndugai wakati akimtangaza.

Baada ya uteuzi huo, Bulaya alisema hakupewa nafasi hiyo kimizengwe kwa kuwa awali alikuwa msaidizi wa Lissu na kwa nafasi yake ya Waziri Kivuli wa Sera, Uratibu na Bunge.

"Nimekuwa mbunge kwa vipindi viwili na sasa kuna vitu vingi navijua hasa masuala ya nidhamu na kanuni za Bunge. Nikiwa mnadhimu, jukumu langu la kwanza ni kuhakikisha Bunge linaendeshwa kwa mujibu wa sheria bila upendeleo, lakini kikubwa ni kuhakikisha maslahi ya Kambi Rasmi ya Upinzani yanazingatiwa.

"Kuna suala la nidhamu kwa wabunge, suala la wao kuwapo bungeni kwa wakati wote, nitahakikisha wanaingia kutimiza wajibu wao kwa kuchangia," alisema.

Bulaya alieleza mambo mengine atakayoyasimamia ni kuwabana wabunge kuwahi bungeni na kujiandaa kwa sababu Bunge la 11 ni la vyama vingi na wanataka kushindana kwa hoja ambazo zimeshiba.

Alisema kutokana na aina ya wabunge wa upinzani waliopo, hana wasiwasi na viwango vyao wabunge wake.

SALAMU KWA MHAGAMA

"Wito wangu kwa mnadhimu mwenzangu wa upande wa serikali (Jenista Mhagama) ni kwamba mimi na yeye pamoja na kiti cha Spika ndio tutafanya pamoja ama Bunge litulie au lisitulie. Mimi na yeye bila kujali masuala binafsi, tunapaswa kuhakikisha haki inatendeka.

"Sasa kumekuwa na utaratibu wa kupindisha tafsiri za kanuni kuonyesha kwamba kuna mbunge fulani amefanya kosa kwa jinsi ambavyo anaona, lakini ukifuata kanuni au tafsiri hicho kitu kinakuwa hakipo kwa sababu wengi wanaazimia kwa sababu ni wengi bila ya kuangalia kanuni zinavyotaka," alisema.

Bulaya aliweka wazi kwamba tayari amejizatiti na yuko imara na anajua wajibu wake na nini anatakiwa kufanya kwa maslahi ya Watanzania na kwa maslahi ya nchi yake, huku akiwataka kutegemea utumishi uliotukuka.

Januari 13, mwaka huu, Mbunge wa Rombo (Chadema), Joseph Selasini alijiuzulu wadhifa huo wa aliokuwa anakaimu baada ya kumwandikia barua Kiongozi Rasmi wa Kambi ya Upinzani Bungeni (KUB), Freeman Mbowe.

Selasini alitoa sababu za kujiuzulu kwake ni kutokana na kile alichoeleza ni kutotambulishwa rasmi kwa uongozi wa Bunge tangu ateuliwa miaka miwili iliyopita.

Selasini alidai kwa wakati huo kwamba alikuwa akiulizwa mara kwa mara na Katibu wa Bunge juu ya barua ya kumtambulisha ili apate fursa ya kuhudhuria vikao vya kikanuni, lakini Mbowe hajawahi kuliandikia Bunge.

Selasini aliteuliwa kukaimu wadhifa huo miaka miwili iliyopita, kutokana na aliyekuwa akishikilia wadhifa huo, Lissu, kuwa katika matibabu nje ya nchi baada ya kushambuliwa kwa zaidi ya risasi 30 na watu wasiojulikana Septemba 7, 2017 nyumbani kwake jijini Dodoma.

Tangu ashambuliwe, Lissu ambaye alikuwa Mbunge wa Singida Mashariki, hakurejea nchini na mwaka jana Bunge lilitangaza kuwa amepoteza sifa ya kuwa mbunge baada ya kushindwa kujaza taarifa za mali na madeni na Spika wa Bunge, Job Ndugai kutojua mahali aliko.

## HABARI KITAIFA

# Mahakama Kuu yatoa maelekezo maridhiano familia Bilionea Msuya

Na allan Isack, ARUSHA

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Arusha, imetoa miezi miwili kwa pande mbili za familia ya aliyekuwa mfanyabiashara, marehemu Erasto Msuya maarufu kama 'Bilionea Msuya', zenye mgogoro wa kugombea mali za mfanyabiashara huyo kukaa meza moja kuondoa tofauti.

Kadhalika, Mahakama hiyo imezielekeza pande hizo kupeleka mrejesho mahakamani baada ya muda huo kupita.

Akitoa uamuzi huo, Jaji wa Mahakama hiyo, Johannes Masara, alisema mahakama imeridhia ombi la upande wa mleta maombi Ndeshukulwa Msuya, la kuomba mahakama kuondoa shauri lake la mirathi kwa muda ili familia hizo zifanye mazungumzo.

Alisema mahakama baada ya kupokea ombi la mleta maombi, imekubali pande hizo, kukaa meza moja kupitia Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, na imetoa miezi miwili kupata mrejesho.

Akizungumza na waandishi wa habari nje viwanja vya mahakama, Ndeshukurwa alisema uamuzi wa mahakama umetenda haki, na umezingatia maslahi mapana ya pande zote mbili na anaamini jambo hilo, litamalizika na watoto wa Bilionea Msuya watapata haki yao ya msingi.

Alisema suala la maridhiano liliibuliwa na DC Muro na aliwataka ndugu hao, waondoe kesi iliyopo mahakamani ili wakae meza moja ya mazungumzo, na aliahidi kusaidia kusimamia mazungumzo hayo.

Awali, wakili wa upande wa wajibu maombi, Shilinde Ngalula, alipinga hatua ya mahakama hiyo kukubali ombi la kuondoa kesi hiyo, kwa muda na alitaka mahakama ifute kabisa kesi hiyo, na kusiwapo shauri hilo, mahakamani wakati wa maridhiano nje ya mahakama.

Hata hivyo, Jaji Masara alikataa ombi hilo, na kukubali ombi la upande wa waleta maombi la kuondoa kesi hiyo kwa muda bila kuifuta kisha kurejea meza ya mazungumzo na iwapo familia hizo hazitakubaliana watarejea mahakamani kuendelea na shauri hilo kwa ajili ya kutolewa uamuzi.

Ndeshukurwa, mama mzazi wa Bilionea Msuya anapinga Miriamu Mrita, ambaye ni mke wa Msuya kuwa msimamizi wa mirathi, akidai kuwa ameshindwa kugawanya mali za mumewe kwa wanufaika kwa kipindi cha miaka saba tangu kifo cha Msuya.

Bilionea Msuya aliuawa kwa kupigwa risasi zaidi ya 20 mwaka 2013 wilayani Hai, mkoani Kilimanjaro.

Ndesgukurwa anadai kwamba Miriamu ambaye ndiye msimamizi wa mirathi, yuko mahabusu gerezani kwa muda mrefu akikabiliwa na kesi ya mauaji ya wifi yake, Anet Msuya, hivyo hatua hiyo imesababisha baadhi ya mali za Bilionea Msuya kupotea na watoto wake kushindwa kupatiwa mgawanyo wa mali zao.

## NHC yatangazia kiama wadaiwa sugu

Na Mwandishi Wetu

SHIRIKA la Nyumba la Taifa (NHC) limetangaza kuanza kuwachukulia hatua wapangaji ambao ni wadaiwa sugu ikiwamo kuwaondoa kwenye nyumba na kukamata mali zao na kuzinadi.

Sambamba na hilo, shirika pia limesema litafanya tathmini ya mikataba iliyoingiwa kati yake na wabia ili kuona kama inafuatwa kwa mujibu wa makubaliano ili kuondoa sintofahamu kati ya pande husika.

Mkurugenzi Mkuu wa NHC, Dk. Maulid Banyani, alisema jana akiwa katika ziara kwenye mkoa wa NHC Temeke kukagua miradi ya shirika iliyoingia mkataba na wabia, huku akiwataka wapangaji wote wanaodaiwa kulipa malimbikizo kabla ya kufikiwa na zahama hiyo.

Alisema katika kutekeleza hilo, shirika halitakuwa na huruma na wapangaji ambao wamekuwa hawatekelezi wajibu wao kwa sababu wanalikosesha shirika fedha ambazo zingefanya shughuli za maendeleo.

"Rai yangu kwa wapangaji ni kuhakikisha wapangaji wote wanalipa kodi kwa wakati na kukamilisha malimbikizo ya kodi wanazodaiwa. Baadhi ya wapangaji wanakiuka taratibu za mikataba yao katika kulipa kodi kwani wamekuwa si waaminifu katika kulipa kodi kwani wamekuwa na malimbikizo makubwa jambo ambalo linakiuka mkataba wa upangishaji walioingia na shirika," alisema.

"Mpangaji wa NHC aliyepanga nyumba ya malazi au eneo la biashara, ana jukumu la kulipa kodi yake kwa wakati kama ambavyo mkataba unamtaka kufanya, lakini baadhi yao wamekuwa wakilimbikiza malipo hayo jambo ambalo ni kinyume cha mkataba waliongia na NHC," alisisitiza.

Katika kutekeleza hilo, alisema shirika halitamwonea haya mpangaji ambaye ana malimbikizo ya kodi kwa kuwa tayari lilishatoa muda kwa wapangaji ambao wana malimbikizo kufika katika ofisi za NHC kwa ajili ya kufanya mazungumzo na kuona namna wanavyokamilisha malipo yao ya kodi wanazodaiwa.

Dk. Banyani alitahadharisha kuwa wapangaji wote ambao hawatakamilisha malipo ya kodi wanazodaiwa, hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao ikiwamo kutangazwa kwenye vyombo vya habari na hatimaye kuwatimua wale watakaoshindwa kulipa.

Katika ukaguzi wa majengo ya ubia yaliyoko katika Mkoa wa Temeke, Dk. Banyani alisema NHC itapita kila jengo ili kuhakikisha taratibu zilizowekwa zinafuatwa na ikiwa umekiukwa, watu hao watafikishwa katika vyombo vya sheria.

Katika hatua nyingine Mkurugenzi Mkuu alisema majengo yote ya ubia yatafanyiwa tathmini upya ili kuona mikataba iliyoingia NHC na wabia hao inafuatwa na kutekelezwa kwa maslahi ya wote bila kuwa na migogoro.




TANGAZO

# BANK OF BARODA (TANZANIA) LTD.

## Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uonyeshaji ya Mwaka 2014)

## WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31.12.2019

**(Kiasi kwa shilingi milion)**

| | | ROBO MWAKA YA SASA | ROBO MWAKA ILIYOPITA 30.09.2019 |
|---|---|---|---|
| A. | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 2,955 | 3,723 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 21,842 | 23,443 |
| 3 | Uwekezaji katika Amana za Serikali | 20,988 | 29,169 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 32,749 | 24,985 |
| 5 | Hundi na Mihamala ya Kushughulikiwa | - | 2 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo iliyotolewa kwa Benki Nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 115,954 | 104,343 |
| 12 | Mali Nyingine | 3,240 | 2,925 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 1,133 | 1,160 |
| 16 | **Jumla ya Mali** | **198,861** | **189,750** |
| B. | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 5,847 | 5,850 |
| 18 | Amana za Wateja | 149,691 | 140,583 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 184 | 397 |
| 23 | Limbikizo la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 38 | 35 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Mihamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 36 | 23 |
| 27 | Dhima Nyingine | 1,873 | 1,523 |
| 28 | Madeni | - | - |
| 29 | **JUMLA YA DHIMA** | **157,669** | **148,411** |
| 30 | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **41,192** | **41,339** |
| C. | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 10,000 | 10,000 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | - | - |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 25,900 | 25,571 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 2,550 | 2,354 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 2,742 | 3,414 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| 37 | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **41,192** | **41,339** |
| 38 | Dhima zisizo Dhahiri | 12,413 | 12,954 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 7,194 | 7,138 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 3,334 | 2,227 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| D | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 20.71% | 21.79% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 6.03% | 6.69% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 76.66% | 72.92% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali | 58.31% | 54.99% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 85.33% | 83.53% |
| (vi | Ongezeko la Amana | 6.22% | 0.00% |
| (vii | Ongezeko la Mali | 4.80% | 0.00% |

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 DESEMBA 2019

**(Kiasi kwa shilingi milion)**

| | | ROBO YA MWAKA SASA 31.12.2019 | ROBO YA MWAKA LINGANISHI 31.12.2018 | LIMBIKIZO LA MWAKA WA SASA 31.12.2019 | LIMBIKIZO LA MWAKA LINGANISHI 31.12.2018 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 4,013 | 3,262 | 14,811 | 13,582 |
| 2 | Gharama za Riba | 1,293 | 1,218 | 4,843 | 4,676 |
| 3 | **Mapato halisi ya Riba (1 kutoa 2)** | **2,720** | **2,044** | **9,968** | **8,906** |
| 4 | Madeni Viza yaliyofutwa | - | - | - | 1,259 |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 1,106 | 606 | 2,216 | 1,018 |
| 6 | **Mapato yasiyo ya Riba:** | **572** | **569** | **1,906** | **1,932** |
| | 6.1 Faida/Hasara zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 142 | 54 | 618 | 349 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 428 | 464 | 1,278 | 1,519 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 2 | 51 | 10 | 64 |
| 7 | **Gharama Zisizo na Riba:** | **1,623** | **1,618** | **5,644** | **5,063** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 656 | 712 | 2,427 | 1,869 |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | 216 | 51 | 479 | 441 |
| | 7.3 Gharama Nyingine | 751 | 855 | 2,738 | 2,753 |
| | 7.4 Other Provision | - | - | - | - |
| 8 | **Faida/(Hasara) ya Uendeshaji** | **563** | **389** | **4,014** | **3,498** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | 366 | 263 | 1,464 | 1,351 |
| 10 | **Faida/(Hasara) ya Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **197** | **126** | **2,550** | **2,147** |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainishi)** | - | - | - | - |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **197** | **126** | **2,550** | **2,147** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | **50** | **48** | **50** | **48** |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 20 | 13 | 255 | 215 |
| 15 | **Idadi ya Matawi** | 4 | **4** | **4** | **4** |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.38% | 0.68% | 1.35% | 2.00% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 1.69% | 3.08% | 6.11% | 6.93% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 49.63% | 55.77% | 47.52% | 47.00% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 6.94% | 1.62% | 6.24% | 5.00% |

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO ILIYOISHIA 31.12.2019

**(Kiasi kwa shilingi milion)**

| | | ROBO YA MWAKA YA SASA 31.12.2019 | ROBO YA MWAKA ILIYOPITA 30.09.2019 | LIMBIKIZO LA MWAKA WA SASA 31.12.2019 | LIMBIKIZO LA MWAKA LINGANISHI 31.12.2018 |
|---|---|---|---|---|---|
| I | Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | 563 | 926 | 4,014 | 3,490 |
| | Marekebisho kwa ajili ya: | | | | |
| | -Hasara katika Mali | 1,150 | 376 | 2,404 | 1,246 |
| | -Prior Period Adjustment | (344) | (70) | (413) | (211) |
| | -Badiliko Halisi Katika Mikopo | (12,718) | (1,351) | (19,597) | (13,583) |
| | -Faida/Hasara kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | 4 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Amana | 9,108 | 9,700 | 17,533 | 6,566 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 150 | 1,723 | 5,614 | (3,157) |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 10,022 | (2,179) | 4,810 | 7,451 |
| | -Kodi Iliyolipwa | (366) | (366) | (1,464) | (1,351) |
| | *-Mengineyo (Bainisha)* | (646) | 1,230 | (646) | (400) |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa(tumika) kwa Shughuli za Uendeshaji** | **6,919** | **9,989** | **12,254** | **55** |
| II | Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji: | | | | |
| | -Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| | -Ununuzi wa Mali za Kudumu | (17) | - | (42) | (45) |
| | -Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | 5 |
| | -Ununuzi wa Amana zisizoshughulikiwa na Mawakala | 8,181 | (1,428) | 2,379 | (6,035) |
| | -Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | *-Mengineyo (ainisha)* | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa(zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **8,164** | **(1,428)** | **2,337** | **(6,075)** |
| III | Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli Kifedha: | | | | |
| | -Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | -Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | -Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | -Gawio Lililolipwa kwa Fedha Tasilimu | - | - | - | - |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| | *-Mengineyo (Bainisha)* | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) Kwa Shughuli za Kifedha** | **-** | **-** | **-** | **-** |
| IV | Fedha tasilimu na Mali Zinazofanana na Fedha Tasilimu: | | | | |
| | -Ongezeko/ punguzo Halisi Katika Fedha Tasilimu na Mali Zinazofanana na Fedha Tasilimu | **15,083** | **8,561** | **14,591** | **(6,020)** |
| | -Fedha Tasilimu na Mali zinazofanana na Fedha Tasilimu Mwanzoni mwa Robo/Mwaka | 30,815 | 22,255 | 31,307 | 37,327 |
| | -Fedha Tasilimu na Mali zinazofanana na Fedha Tasilimu Mwanzoni mwa Robo/Mwaka | **45,898** | **30,815** | **45,898** | **31,307** |

## TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31.12.2019

**(Kiasi kwa shilingi milion)**

| | Mtaji wa Hisa | Malipo Juu ya Bei ya Hisa | Mapato yaliyo Bakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineya (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **MWAKA WA SASA** | | | | | | | |
| **Salio la Mwanzo wa Mwaka** | **10,000** | **-** | **24,134** | **3,984** | **937** | **-** | **39,055** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 2,550 | - | - | - | 2,550 |
| Mapato Mengineyo yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 1,242 | (1,242) | - | - | - |
| Tengo la ziada ya Jumla | - | - | 937 | - | (937) | - | - |
| Mengineyo | - | - | (413) | - | - | - | (413) |
| **Salio la Mwisho wa Mwaka** | **10,000** | **-** | **28,450** | **2,742** | **-** | **-** | **41,192** |
| **MWAKA ULIOPITA** | | | | | | | |
| **Salio la Mwanzo wa Mwaka** | 10,000 | - | 22,271 | 4,068 | 781 | - | 37,120 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 2,147 | - | - | - | 2,147 |
| Mapato Mengineyo yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 84 | (84) | - | - | - |
| Tengo la ziada ya Jumla | - | - | (156) | - | 156 | - | - |
| Mengineyo | - | - | (212) | - | - | - | (212) |
| **Salio la Mwisho wa Mwaka** | **10,000** | **-** | **24,134** | **3,984** | **937** | **-** | **39,055** |

**BAADHI YA MAELEKEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31.12.2019**

**Katika Kuandaa taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za Mwaka uliopita. (Mabadiliko katika sera za uandaaji wa taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya /mwaka wa sasa, yaelezwe kwa mujibu wa ISA 34 na ISA 8)**

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Rajendra Sadashiv Mohrir<br>(Mkurugenzi Mtendaji) | | 13th January, 2020 |
| Deogratias Edward Ndushi<br>Mkuu wa Fedha | | 13th January, 2020 |
| Mwita Mohamed Mwita<br>(Mkaguzi wa Ndani) | | 13th January, 2020 |

**Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya Kimataifa vya Uwasirishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya Mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.**

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Dkt. Proches Meshili Kiwango Ngatuni | | 13th January, 2020 |
| Dkt. Emmanuel Sadiki | | 13th January, 2020 |

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Udhibiti mawakala vyuo vya nje uwe endelevu

**KWA** miaka kadhaa yamekuwapo malalamiko kuhusiana na wimbi la mawakala ambao wamekuwa wakiwashawishi wazazi kuwa wanapeleka wanafunzi nje ya nchi kwa ajili ya elimu ya juu.

Kuwapo kwa kampuni nyingi zinazodai kuwa mawakala wa kupelea wanafunzi nje ilifika wakati ikaonekana kuwa ni bughudha na usumbufu kwa kuwa nyingi ilifika mahali zikaonekana za kitapeli.

Hali hiyo ilitokana na wanafunzi wengi waliopelekwa nje kwa njia hizo kujikuta katika wakati mgumu, kutokana na kutelekezwa huko na kuhangaika.

Walikuwa wakikutwa na majanga hayo kutokana na kampuni zilizowapeleka kutowaeleza ukweli ikiwamo gharama halisi wanazotakiwa kutoa, badala yake kuwalaghai kuwa wangetoa fedha zilizo kwenye uwezo wao.

Kadhalika, wajanja hao pengine kutokana na serikali kutokuwa na mfumo thabiti wa udhibiti, walikuwa wanawapeleka baadhi ya wanafunzi kwenye vyuo ambavyo havitambuliki, hivyo baada ya kuhitimu na kurejea nchini wanajikuta wakiambiwa na mamlaka husika kuwa vyeti vyao havitambuliki.

Kimsingi, wahitimu kadhaa waliosoma ng'ambo walijikuta wakikosa ajira ama fursa za kudahiliwa na vyuo vya elimu ya juu nchini kwa ajili ya masomo zaidi.

Taarifa za kutia moyo ni kuwa hatua iliyochukuliwa na serikali ya kudhibiti mawakala hao imeonyesha kuanza kuzaa matunda, baada ya kupunguza kampuni hizo kwa kiwango kikubwa.

Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), imesema kwamba imewadhibiti mawakala makanjanja wanaojihusisha na udahili wa wanafunzi wanaokwenda kusoma vyuo nje ya nchi.

Hayo yalibainishwa jana jijini Dar es Salaam na Katibu Mtendaji wa TCU, Prof. Charles Kihampa, alipokuwa akizungumzia mafanikio ya taasisi yake katika kipindi cha uongozi wa serikali ya Rais John Magufuli, na kubainisha kwamba mpaka sasa mawakala wanaotambulika wapo watatu.

Alisema kwa muda wa miaka 12, wamekuwapo mawakala wanaodahili wanafunzi wanaokwenda vyuo vya nje ya Tanzania bila ya kufuata utaratibu uliowekwa.

Prof. Kihampa alisema jukumu mojawapo la TCU ni kuzisajili wakala hizo, lakini haikuwahi kufanyika akitaja sababu mojawapo ni kukosekana kwa miongozo ya namna bora ya kuzitambua na taratibu za uendeshaji.

Alisema TCU imeweza kuiandaa miongozo hiyo na mpaka sasa wakala zilizoomba usajili na kukidhi kiwango na kusajiliwa ni tatu ambazo ni kampuni ya Global Education Link, DARWIN Education Agency na Yuhoma Education.

Alisema wakala zingine tatu ambazo ziliomba kusajiliwa hazikuweza kukidhi sifa stahili, ingawa hakuzitaja, na kuongeza kuwa ambazo zimesajiliwa zitatakiwa kuhuisha usajili wake kila baada ya miaka mitatu.


Alisema mwezi huu wamepokea maombi ya wakala wengine saba na taratibu za usajili zinaendelea. Alisema TCU imefanikiwa kuimarisha mifumo yake ya kielektroniki, na kwamba mfumo wa kutathmini uhalali wa vyeti vya wahitimu wanaotunukiwa tuzo na vyuo vya nje ya nchi hufanyika ndani ya siku tatu, tofauti na awali siku 14.

Kwa mujibu wa Prof. Kihampa, katika kipindi hiki zaidi ya vyeti 8,328 vimehakikiwa na kufanyiwa utambuzi. Hatua ambayo tunaona kuwa ina manufaa kwa taifa, kwa kuwa itasaidia kuwanusuru wanafunzi waliokuwa wanakimbilia kujiunga na vyuo vya nje bila kuangalia ubora wa elimu inayotolewa sambamba na kuepuka kutapeliwa.

Ushauri wetu kwa TCU ni kuwa iweke mfumo au dawati la kutoa ushauri kwa wazazi na wanafunzi wanaotaka kwenda kusoma ng'ambo ili kujua ukweli kuhusu vyuo wanavyokusudia kama inavitambua.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Hospitali Mloganzila kasoro hizi zinazaa kero kubwa

Na Beatrice Moses

**HOSPITALI** ya Taifa Muhimbili(MNH)tawi la Mloganzila inatajwa kuwa miongoni mwa taasisi za afya zenye majengo mazuri na mazingira ya kuvutia hasa Afrika Mashariki.

Katika hospitali hiyo kama ilivyo kwa taasisi yoyote ya kisasa inakuwa na mambo mengi muhimu ambayo huyazingatia, ikiwamo usafi wa mazingira, ulinzi na usalama wa wagonjwa na jamii nzima ya eneo kwa ujumla.

Ni wazi kwamba, taasisi hii inatarajiwa kutoa huduma zake kwa kiwango cha kimataifa kulingana na hadhi yake. Lakini nami nina ushuhuda wangu kuhusu nilivyoviona huko, ambavyo kwa maoni yangu inapaswa kushughulikiwa.

Hivi karibuni nilijikuta nalazimika kuyafahamu mazingira na taratibu za taasisi hiyo, baada ya kuwa na mgonjwa aliyelazwa katika hospitali hiyo.

Miongoni mwa taratibu zilizoweka na hospitali ni pamoja na muda wa kuruhusiwa kuingia wodini kumuona mgonjwa, imepangwa asubuhi na jioni, kwa ndugu jamaa na mrafiki waNaruhusiwa kuwaona wagonjwa wao.

Pia saa 6.00 mchana kuna ruhusa, lakini maalum kwa ndugu au jamaa mmoja aliye na chakula kwa mgonjwa. Anaruhusiwa kuingia baada ya ukaguzi.

Nimelazimika kuliandika hili, kutokana na niliyoyaona katika utaratibu wa hospitalini, nadhani kuna haja ya kuyaboresha, ili kuondoa kero kwa ndugu na jamaa wanaofika kuona wagonjwa hopitalini.

Utaratibu wa kuingia kuwaona wagonjwa unasimamiwa na askari wa ulinzi kutoka Suma JKT, wakiwa na utaratibu wa kuwakagua ndugu na jamaa, jambo ambalo ni njema kwa masuala ulinzi na usalama.

Shida inayojitokeza, ni baadhi ya askari hao kutokuwa makini na ukaguzi huo, ambao unafanyika wakati wanaingia na wanapotoka wodini, hali inayozua usumbufu na unaweza kusababisha vurugu isiyo na tija .

Ndugu au jamaa anapokaguliwa, haelezwi kipi ama anapaswa au hapaswi kuingia nacho wodini. Nilishuhudia mmoja wa ndugu wa mgonjwa akisumbuliwa, baada ya kutoka kuona mgonjwa wake na akakaguliwa tena akakutwa na kompyuta mpakato (Laptop).

Hapo askari wa kike akamuhoji kama aliandikisha wakati anaingia nayo wodini, ndugu yule akajibu hapana. Akaeleza hakujulishwa na aliyemkagua wakati anaingia na kama alipaswa kuandika kama ana Laptop hiyo.

Askari yule wa kike maneno yakaanza kumtoka "tutaaminije kuwa ni yako? Kwa nini hukuandikisha? Hapa kuna laptop za wanafunzi tutajuaje kama hii siyo yao?" Ndugu huyo wa mgonjwa naye akahamaki.

Bahati nzuri askari mwingine ambaye nilibaini kuwa alikuwa ni kiongozi, aliamua kuingilia kati kwa kuamuru ndugu wa mgonjwa aandike kwenye daftari, kisha aondoke kuendelea na shughuli zake.

Binafsi nilijikuta najiuliza jinsi gani ambavyo uzembe wa askari aliyemkagua mara ya kwanza ndugu huyo, umesababisha usumbufu, lakini pia nikajiuliza ingekuwaje kama ingekuwa ni silaha?

Pia, usumbufu mwingine ni wakati wa kuingia jioni. Utaratibu uliopo ni tofauti na asubuhi. Muda huo, lazima ndugu apatiwe kadi maalumu anayopaswa kuionyesha katika lango kuu la kuingilia jengo la hospitali.

Utaratibu huo unasimamiwa na askari na ndugu wanatakiwa kukaa chini mahali hapo, ambako kuna 'vimbweta'vilivyojengwa lakini ni vichache hivyo havitoshelezi watu wote kukaa.

Katika hali ya kushangaza askari huamuru watu wakae chini kwenye sakafu ndipo awape kadi, wale wanaogoma kukaa huwanyima.

Kwa siku kadhaa ambazo mgonjwa wangu alikuwa hapo nimeshuhudia malalamiko mengi, kuna Profesa mmoja wa chuo kikuu jina nalihifadhi aliamua kuondoka bila kwenda kusalimia mgonjwa wake kutokana na kugoma kukaa chini.

Ni kama vile adhabu fulani hivi unapaswa kuitekeleza ili kupewa kadi hiyo, askari ajali umri, unadhifu wala hali ya mtu anayemuamuru kukaa chini anachotaka ni utekelezaji.

Katika kile kinachoonekana kadi hizo ni chache, hivyo askari akikawa zikiisha hulazimika kuzifuata kwenye mlango mkuu wa kuelekea geti ambapo ndipo ukaguzi hufanyika na kadi huachwa hapo, kisha kuchukuliwa na kuzigawa kwa ndugu wengine.

Naamini kuwa askari wa Suma JKT waliopo katika Hospitali hii watapata nafasi ya kutafakari huduma wanayoitoa, kisha watachukua hatua kuhakikisha wanaboresha ili kuondoa kero kwa wanaofika kuwaona wagonjwa.

Kero nyingine ni uchafu wa baadhi ya watu wanaofika kuwaona wagonjwa, hawajali juhudi za dhati zinazofanywa na uongozi wa hospitali hiyo kutunza mazingira.

## HABARI PICHANI


# ZIARA YA MKURUGENZI MTENDAJI WA BENKI YA UBA VYOMBO VYA HABARI VYA IPP



Kaimu Mhariri Mtendaji wa gazeti la The Guardian, Richard Mngazija (katikati), akitoa maelezo kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya UBA, Usman Imam Isiaka (wa pili kulia), kuhusu maandalizi ya gazeti, wakati alipotembelea vyombo vya habari vya IPP, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Kaimu Mhariri Mtendaji wa gazeti la Nipashe, Epson Luhwago. PICHA ZOTE: SELEMAN MPOCHI



Meneja Uchapaji wa kampuni ya magazeti ya The Guardian Ltd, Balasabramanian (katikati), akifafanua jambo kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya UBA, Usman Imam Isiaka, alipotembelea kiwanda cha uchapishaji cha kampuni hiyo.



Balasabramanian (wa pili kulia), akionyesha jinsi magazeti yanavyochapwa.



Mratibu wa vipindi wa East Africa Television, Sophia Mng'anya akimfafanulia jambo mkurugenzi huyo, Usman Imam Isiaka.



Mkurugenzi wa Chaneli za ITV, Koigi Macharia, akimweleza Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya UBA, Usman Imam Isiaka, jinsi matangazo yanavyorushwa.



Mkurugenzi wa Chaneli za ITV, Koigi Macharia akimweleza Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya UBA, Usman Imam Isiaka, jinsi taarifa ya habari inavyorushwa.

# Washtakiwa mauaji ya Dk. Mvungi wamkataa hakimu

**Na Hellen Mwango**

WASHTAKIWA wanaokabiliwa na kesi ya mauaji ya aliyekuwa Mjumbe wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba, Dk. Sengodo Mvungi, wamemwomba hakimu kurejesha jalada la kesi yao kwa Hakimu Mfawidhi kwa sababu hawana imani naye.

Washtakiwa hao waliwasilisha hoja hiyo jana mbele ya Hakimu Mkazi, Vicky Mwaikambo, aliyepangiwa kusikiliza usikilizwaji wa awali wa kesi hiyo katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam.

Wakili wa Serikali, Ashura Mzava, alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo haujakamilika, hivyo kuomba tarehe nyingine ya kutajwa.

Kutokana na kauli hiyo, mshtakiwa Longishu Losingo alinyoosha mkono akaomba kuzungumza, aliporuhusiwa alidai kesi yao ni ya muda mrefu, lakini hakuna kinachoendelea, hivyo wanateseka mahabusu.

"Tunaomba mheshimiwa hakimu ulirudishe jalada la kesi yetu kwa mfawidhi, hatuna imani na wewe ili apangiwe hakimu mwingine," alidai Losingo.

Hakimu Mwaikambo alisema amesikia hoja za utetezi, aliwataka waandike barua ya kutokuwa na imani kwenda kwa hakimu mfawidhi.

Alisema kesi hiyo itatajwa Februari 10, mwaka huu.

Awali, upelelezi ulikamilika na baadhi ya washtakiwa waliachiwa mwaka 2018, jalada lilikwenda Mahakama Kuu kwa ajili ya kuanza kusikilizwa.

Hata hivyo Novemba 11, 2018 kesi iliondolewa, washtakiwa walirudi kituoni na kushtakiwa upya katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu.

Washtakiwa ni pamoja na Msigwa Matonya (35), Mianda Mlewa (45), Paulo Mdonondo (35), Longishu Losindo (34), Juma Kangungu (34) na John Mayunga (60), walipanda kizimbani jana Jumanne Juni 18, 2019.

Katika kesi ya msingi, washtakiwa hao kwa pamoja wanakabiliwa na shtaka la mauaji ambapo inadaiwa kuwa Novemba 3, mwaka 2013, walifanya kosa la mauaji ya kukusudia kinyume na kifungu cha 196 cha sheria na kanuni ya adhabu sura ya 16 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2002.

Ilidaiwa kuwa siku hiyo ya tukio katika eneo la Msakuzi Kiswegere lililoko eneo la Wilaya ya Kinondoni, washtakiwa hao kwa pamoja walimuua kwa kukusudia Dk. Sengondo Mvungi ambaye alikuwa Mjumbe wa Kamati Kuu ya NCCR-Mageuzi.


Land Form No. 54 A

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

THE LAND ACT, 1999
(No. 4 of 1999)
DEFAULT NOTICE
(Under Section 127)

**Certificate of Occupancy No. 119466 located on plot number 308 block "C" at Tegeta, Dar es salaam.**
**Certificate of occupancy No. 91795 located on plot number 6 block 'C' at Mapinga, Bagamoyo urban area.**

**To: PROSPER PAUL MASSAWE**
**Dar essalaam.**

Be notified of the default to honour your obligations, covenanted under the mortgage with Maendeleo Bank PLC, whereby **you guaranteed NANGEDA 1982 INTERNATIONAL LTD who have failed to repay a credit facility extended to by Maendeleo Bank PLC** to the extent that the outstanding debt as at **27.01.2020** was **TZS. 276,097,734.38/=** arising from a loan facility granted to **NANGEDA 1982 INTERNATIONAL LTD** by Maendeleo Bank PLC.

You are hereby required to pay the said **TZS. 276,097,734.38/=** so as to rectify the said default.Please be informed that penalties and interest accrues daily.

Be further notified that in the event you do not rectify the default stated above within Sixty (60) days from receipt of this notice, we may exercise our right to sell the mortgaged property/land registered in our favor, or appoint a receiver, or lease the property, or enter possession or sue you in court with costs.

Dated at Dar es Salaam this ........ day of ......... 2020.

MAENDELEO BANK Together in Progress MAENDELEO BANK LTD P. O. BOX 216, DAR ES SALAAM

**FOR MAENDELEO BANK TANZANIA LIMITED**

Served upon me at Dar es Salaam this ..........day of ......., 2020

.........................................
**Signature of Borrower/Spouse/Local Government/Guarantor**




Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mussa Azzan 'Zungu', akipokea shada la maua kutoka kwa Mwenyekiti wa CCM, Kata ya Kivukoni, Sharik Choughle, wakati akiwasili katika ofisi za wizara hiyo, jijini Dar es Salaam jana, baada ya kuapishwa kushika nafasi hiyo, juzi. Wa pili kulia ni Naibu Waziri wa wizara hiyo, Mussa Sima na (kulia) Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu wa wizara hiyo, Emma Limo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Upelelezi wapiga kalenda kesi mamilioni ya mbunge

**Na Gideon Mwakanosya, SONGEA**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Ruvuma imeahirisha kesi inayomkabili mfanyabiashara wa duka la pembejeo, Cosmas Haule, anayetuhumiwa kwa wizi wa kuaminika dhidi ya Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Jacqueline Ngonyani wa Sh. milioni 440.

Kesi hiyo imeahirishwa hadi Februari 13, mwaka huu baada ya upande wa mashtaka kudai kuwa upelelezi wa kesi hiyo haujakamilika.

Wakili wa serikali toka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu Kanda ya Songea, Hellen Chuma, aliiomba mahakama kupanga tarehe nyingine kwa sababu upelelezi haujakamilika.

Kufuatia hali hiyo, Hakimu wa Mahakama hiyo, Cleophance Waane, alilidhia kupanga tarehe nyingine kwa kuwa upande wa utetezi haukuwa na pingamizi.

Inadaiwa kuwa Haule ambaye ni mfanyabiashara wa duka la pembejeo katika Manispaa ya Songea, alitenda kosa la wizi wa kuaminika dhidi ya mbunge huyo kiasi hicho cha fedha kati ya Novemba 27, 2015 hadi Desemba mwaka jana katika benki ya CRDB tawi la Songea.

Inadaiwa kuwa Ngonyani alimpatia Cosmas kiasi hicho cha fedha ili amhifadhie kwenye akaunti yake, lakini mshtakiwa huyo alizitumia tofauti na makubaliano waliyoingia.

Hata hivyo, mshtakiwa alikana kutenda kosa hilo na yupo nje kwa dhamana.

# Mawakala makanjanja wa wanafunzi nje wadhibitiwa

**Na Romana Mallya**

TUME ya Vyuo Vikuu nchini (TCU) imesema imewadhibiti mawakala makanjanja wanaojihusisha na udahili wa wanafunzi wanaokwenda kusoma vyuo nje ya nchi.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Katibu Mtendaji wa TCU, Prof. Charles Kihampa, kuhusu mafanikio yao katika kipindi cha uongozi wa serikali ya Rais John Magufuli, alisema mpaka sasa mawakala wanaotambulika wapo watatu.

Alisema kwa muda wa miaka 12 wamekuwapo mawakala wanaodahili wanafunzi wanaokwenda vyuo vya nje ya Tanzania bila ya kufuata utaratibu uliowekwa.

"Jukumu mojawapo la TCU ni kuzisajili wakala hizi, lakini haikuwahi kufanyika, sababu mojawapo ilikuwa ni kukosekana kwa miongozo ya namna bora ya kuzitambua na taratibu za uendeshaji," alisema Prof. Kihampa.

Alisema TCU imeweza kuiandaa miongozo hiyo na mpaka sasa wakala zilizoomba usajili na kukidhi kiwango na kusajiliwa ni tatu ambazo ni kampuni ya Global Education Link, DARWIN Education Agency na Yuhoma Education.

"Wakala wengine watatu ambao waliomba kusajiliwa hazikuweza kukidhi sifa stahili. Hizi ambazo zimesajiliwa zitatakiwa kuhuisha usajili wake kila baada ya miaka mitatu," alisema Prof. Kihampa.

Alisema ndani ya mwezi huu wamepokea maombi ya wakala wengine saba na taratibu za usajili zinaendelea.

"Wakala ambao hawajasajiliwa wanahimizwa kutuma maombi yao, kuendesha wakala wa udahili bila usajili ni kinyume cha kanuni, wananchi watumieni mawakala wanaotambuliwa na TCU," alisema Prof. Kihampa.

Prof. Kihampa alisema TCU imefanikiwa kuimarisha mifumo yake ya kielektroniki na kwamba mfumo wa kutathmini uhalali wa vyeti vya wahitimu wanaotunukiwa tuzo na vyuo vya nje ya nchi hufanyika ndani ya siku tatu, tofauti na awali siku 14.

Alisema katika kipindi hiki zaidi ya vyeti 8,328 vimehakikiwa na kufanyiwa utambuzi.

"Uhakiki wa vyeti kwa wahitimu hawa wanaosoma nje ya nchi unawapa fursa wananchi kufahamu uhalali wa vyuo na programu wanazokwenda kusoma na kuwaepusha na hasara ya kupoteza rasilimali fedha na muda," alisema Prof. Kihampa.

HABARI KITAIFA

# DC amsweka ndani mkuu wa chuo kwa tuhuma nzito

**Na Sabato Kasika**

MKUU wa Wilaya ya Kilolo mkoani Iringa, Asia Abdallah, amemweka ndani Mkurugenzi wa Chuo cha Maendeleo ya Uongozi kilichopo kijiji cha Katowo, kwa tuhuma za utapeli.

Katika taarifa yake kwa vyombo vya habari, mkuu wa wilaya amemtaja mkurugenzi huyo kwa jina moja la Mhema na kusema, alikamatwa na vyombo vya dola tangu Jumatano wiki ya iliyopita.

Aidha, ameutangazia umma kwamba wanafunzi na wananchi wote wenye malalamiko na chuo hicho wafike kituo cha polisi Mbigiri, Kilolo kuandikisha madai yao ili sheria ichukua mkondo wake.

Mkuu huyo wa wilaya alisema aliongoza kamati kusikiliza kilio cha wanafunzi wa chuo hicho na wanakijiji wa Katowo na kufikia uamuzi wa kumtia ndani.

"Chuo hicho kilianzishwa mwaka 2017 kwa kupokea wanafunzi wa cheti, kikiwa bado hakijasajiliwa na kilikuwa kikiendeshwa katika majengo ya umma (ghala) na aliendelea kujiongezea majengo likiwamo soko ambalo alivunja muundo wake bila kibali cha vikao halali na kuanza kulitumia kwa kazi za chuo bila makubaliano," alisema Asia.

Alisema wanafunzi wa mwaka 2017 wamekuwa akiwapotezea muda na kuchukua fedha zao huku akijua chuo hakijasajiliwa, na kwamba amewatapeli wanafunzi, kwa vile baada ya kuhitimu hakuwapa vyeti.

"Inaonekana chuo kimesajiliwa 2018, lakini hakijakidhi taratibu, ili kiweze kuendana na masharti ya Nacte, na tulipofuatilia Nacte tumefahamishwa kuwa kimekuwa kikiendeshwa bila kukidhi taratibu," alisema.

Alisema, kutokana na hali hiyo, mhusika aliamuliwa akifunge hadi hapo atakapofuata sheria, kanuni na taratibu, na kwamba alikubali kukifunga, lakini akawa anaendelea kupokea wanafunzi bila kusoma.

"Yaani ni kwamba, pamoja na Nacte kufunga chuo hicho mwaka jana, bado ameendelea kuchukua fedha za wanafunzi huku mwenyewe akiwa amewatelekeza anaishi kwa machale na wanafunzi wamebaki hapo chuoni hawana ratiba ya masomo," alisema.

Alisema, mkurugenzi huyo amekaidi na kupuuza maagizo ya serikali ya kijiji yaliyomtaka akabidhi jengo alilokuwa akitumia kama chuo tangu mwaka jana lakini hadi Januari 22 mwaka huu alikuwa hajatekeleza.

"Mhema na amekabidhiwa kwa polisi kwa hatua za uchunguzi wa madai yote ya kijiji, wanafunzi, walimu, watu wengine wanaomdai na uharibifu alioufanya katika majengo bila makubaliano," alisema.

Alisema, anatakiwa kuhakikisha wanafunzi wote wanapatiwa vyeti, kutoa vifaa vyake vyote na kukabidhi majengo kwa wamiliki halali, asikanyage eneo hilo na atafutie wanafunzi utaratibu mwingine wa kuendelea na masomo yao.

# Mkenya ahukumiwa kwa kukutwa shehena mirungi

**Na Mwandishi Wetu, PEMBA**

RAIA wa Kenya na mkazi wa Kizimbani Wete kisiwani Pemba, Omar Mohamed Juma, amehukumiwa kulipa faini ya Sh. 2,000,000 au kutumikia kifungo cha miaka miwili baada ya kupatikana na maboksi tisa ya dawa za kulevya aina ya mirungi yenye uzito wa gramu 2,100.

Hukumu hiyo ilitolewa na Jaji wa Mahakama Kuu Zanzibar, Abdul-hakimu Ameir Issa, baada ya kumaliza kusikiliza ushahidi wa pande zote mbili na kuona kuwa mtuhumiwa huyo ana kesi.

Alisema mahakama ilisikiliza mashahidi sita ambapo shahidi Fatma Iddi Rashidi, mchunguzi kutoka Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali, alithibitisha baada ya uchunguzi wake kuwa kielelezo alichopewa ni dawa za kulevya aina ya mirungi yenye uzito wa gramu 2,100.

Alisema mashahidi wengine ni nahodha Abdalla Kombo na baharia Makame Faki Haji ambao waliithibitishia mahakama kuwa walimchukua mtuhumiwa Shimoni, Kenya akiwa na begi jeusi mgongoni.

"Waliithibitishia mahakama kuwa walipokwenda kuuza pweza Shimoni, mshtakiwa huyo aliwaomba wamsaidie kwa kuwa anakwenda kwao Pemba, hivyo walimchukua akiwa na begi jeusi mgongoni," alisema Jaji huyo.

Jaji alieleza kuwa mashahidi wengine ni maofisa wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA), Ali Seif Ali na Rajab Abdallah Suleiman ambao waliithibitishia mahakama kukabidhiwa mtuhumiwa aliyekuwa na begi nyeusi mgongoni kutoka kwa askari wa Kikosi cha Kuzuia Magendo (KMKM), Mlingi Mgango Bwire, ambapo askari huyo alitoa ushahidi wa kumkamata mshtakiwa.

Kabla ya kutolewa adhabu hiyo kwa mshtakiwa, Mwendesha Mashtaka kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Pemba, Ali Amour Makame, aliiomba mahakama kutoa adhabu kali kwa mshtakiwa ili iwe fundisho kwake na kwa wengine wenye tabia kama hiyo.

Mshtakiwa aliiomba mahakama impunguzie adhabu kwani ana familia Kenya na kisiwani Pemba ambayo inamtegemea.

Awali mshtakiwa huyo alitenda kosa hilo Mei 5 mwaka 2019 saa 6:00 mchana katika Bandari ya Mawe Matatu Makangale Wilaya ya Micheweni Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Hata hivyo, mshtakiwa alinusurika kwenda jela, baada ya kulipa faini ya Sh. 2,000,000.


JAMHURI YA MUUNGANO TANZANIA
MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA

**ISO 9001:2015 CERTIFIED**

TCRA CREATING A LEVEL PLAYING FIELD

## TAHADHARI KWA UMMA

NDUGU WATANZANIA;

KAMA MNAVYOFAHAMU, LAINI ZA SIMU AMBAZO HAZIJASAJILIWA KWA KUTUMIA NAMBA YA KITAMBULISHO CHA TAIFA **(NIN)** NA KUTHIBITISHWA KWA ALAMA ZA VIDOLE ZILIANZA KUZIMWA TAREHE 20 JANUARI, 2020 USIKU NA **ZOEZI LINAENDELEA.**

**HAKIKI TENA USAJILI WA LAINI ZAKO KWA KUPIGA NAMBA *106# NA UCHUKUE HATUA STAHIKI SASA.**

1.0 KWA WALIOSITISHIWA HUDUMA ZA LAINI ZAO ZA SIMU KUANZIA TAREHE 20.01.2020 WANAWEZA PIA KUENDELEA NA UTARATIBU WA USAJILI KWA LENGO LA AMA KURUDISHA LAINI ZAO ZILIZOFUNGWA KAMA ZITAKUWA BADO ZIPO AU KUPATA LAINI MPYA. **ZOEZI HILI NI ENDELEVU.**

2.0 KWA WATUMIAJI/WAOMBAJI **(WATANZANIA)** WAPYA WA LAINI ZA SIMU WATAENDELEA KUSAJILIWA MUDA WOTE KWA KUTUMIA NAMBA YA KITAMBULISHO CHA TAIFA NA KUTHIBITISHA KWA ALAMA ZA VIDOLE. **HUDUMA HIYO NI ENDELEVU PIA.**

3.0 MATUMIZI SAHIHI YA VITAMBULISHO WAKATI WA USAJILI WA LAINI ZA SIMU(ZINAZOTUMIKA AMA KWA AJILI YA MAWASILIANO YA SIMU ZA SAUTI AU VIFAA VYA MAWASILIANO MENGINE)UKO KATIKA MAKUNDI YAFUATAYO: -

3.1 Sisi wa-**Tanzania** kitambulisho chetu ni kile cha Taifa kitolewacho na NIDA kwa vigezo vyao;

3.2 Kwa wageni wanaokaa hapa nchini **chini ya miezi sita** wanasajili laini za simu kwa kutumia namba za Hati zao za kusafiria na kuthibitisha kwa alama za vidole;

3.3 Kwa wageni wanaokaa **zaidi miezi sita** wanatumia vitambulisho ***(Legal Resident ID)*** ambavyo hupewa na NIDA (Hii ni kwa mujibu wa utaratibu wa idara ya Uhamiaji na NIDA);

3.4 Kwa wanadiplomasia wanatumia Hati zao za kusafiria pamoja na vitambulisho vyao vinavyotolewa na Wizara ya Mambo ya nje; na

3.5 Kwa wakimbizi wanatumia vitambulisho vyao ambavyo hutolewa na NIDA ***(Hii ni kwa mujibu wa utaratibu wa idara ya Uhamiaji na NIDA),***

4.0 KATIKA KUJIRIDHISHA KUWA WALIOSAJILI LAINI ZAO ZA SIMU WAMETUMIA VITAMBULISHO SAHIHI, TCRA KWA KUSHIRIKIANA NA WATOA HUDUMA ITAFANYA ZOEZI LA KUHAKIKI LAINI ZOTE ZITAKAZOKUWA ZIMESAJILIWA ILI KUWAONDOA WALE WALIOSAJILI LAINI ZAO AMA KWA KUTUMIA VITAMBULISHO VYA WATU WENGINE AU KWA KUTUMIA KITAMBULISHO TOFAUTI SAMBAMBA NA KUWACHUKULIA HATUA ZA KISHERIA.

5.0 IKUMBUKWE PIA KWAMBA KUSAJILI LAINI YA SIMU KWA KUTUMIA KITAMBULISHO CHA MTU MWINGINE NI KOSA SANJARI NA KUPEWA LAINI ILIYOSAJILIWA NA MTU MWINGINE.

6.0 **ONYO NA TAHADHARI ZINAENDELEA KUTOLEWA KWA MAKUNDI YOTE YALIYOORODHESHWA KWENYE KIPENGELE CHA 3.0 HAPO JUU, KUTOTUMIA KITAMBULISHO KISICHOKUHUSU WAKATI UNASAJILI LAINI ZAKO ZA SIMU** (ZINAZOTUMIKA AMA KWA AJILI YA MAWASILIANO YA SIMU ZA SAUTI AU VIFAA VYA MAWASILIANO MENGINE).

**ImetolewanaMkurugenziMkuu**
**MamlakayaMawasiliano Tanzania (TCRA)**
**24Januari, 2020**

215600102

HABARI BUNGENI

# Hospitali rufani kupata X-ray tano za kisasa

SERIKALI inatarajia kupeleka mashine za digitali za X-Ray tano katika hospitali za rufani za mkoa.

Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile (pichni), alitoa kauli hiyo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Tunza Malapo.

Katika swali lake mbunge huyo, alihoji ni lini serikali itapeleka X-ray mashine mpya katika Hospitali ya Rufani ya Mtwara-Ligula.

Akijibu swali hilo, Dk. Ndugulile alitaka hospitali hizo ni Mtwara, Njombe, Iringa, Tabora na Temeke.

"Ni kweli Hospitali ya Ligula inakabiliwa na uchakavu wa mashine ya X–ray ambayo huharibika mara kwa mara, katika ziara yangu ambayo niliifanya katika hospitali hii mnamo tarehe 04/12/2018 nilijionea uchakavu wa mashine hiyo na nilitoa ahadi ya serikali ya kuipatia hospitali hii mashine mpya ya digital X-ray," alisema.

Alieleza kuwa mashine tano mpya za X-ray za kidigitali zimeingia nchini kupitia utaratibu wa Managed Equipment Services (MES), Januari 14, 2020.



**"Ni kweli Hospitali ya Ligula inakabiliwa na uchakavu wa mashine ya X–ray ambayo huharibika mara kwa mara, katika ziara yangu ambayo niliifanya katika hospitali hii mnamo tarehe 04/12/2018...**

# Mlinga ahoji gari la mahabusi

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

MBUNGE wa Ulanga (CCM), Goodluck Mlinga (pichani), amesema mahabusi katika Gereza la Ulanga wamekuwa wakibebwa kwa kutumia pikipiki, hali ambayo ni hatari.

Akiuliza swali la nyongeza bungeni jana, Mlinga alisema gereza hilo mwaka wa tano sasa mahabusi wanapelekwa mahakamani kwa kutumia usafiri wa bodaboda ni hatari inaweza kusababisha mahabusu kutoroka.

"Je, lini serikali itapeleka gari la mahabusu Gereza la Ulanga?" Alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yusuf Masauni, alisema serikali inatambua tatizo la usafiri kwa baadhi ya magereza nchini na gari likipatikana litapelekwa katika gereza hilo ili kuondoa tatizo linalowakabili.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Tabora Mjini (CCM), Emmanuel Mwakasaka, alisema kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu ya malimbikizo ya madeni ya wazabuni wanaotoa huduma mbalimbali ikiwapo huduma ya kupeleka chakula kwa wafungwa magerezani na matengenezo ya magari.

Alihoji serikali ina mkakati gani wa kulipa madeni hayo.

Masauni akijibu swali hilo, alisema serikali katika nyakati tofauti imekuwa na mkakati wa kulipa madeni yake ya ndani ikiwamo madeni ya watoa huduma, chakula cha wafungwa na matengenezo ya magari katika Magereza yote nchini.



"Katika mwaka wa fedha 2016/17 hadi 2018/19 jumla ya kiasi cha fedha Sh. bilioni 23.56 kimelipwa kwa ajili ya watoa huduma za uendeshaji, chakula cha wafungwa na matengenezo ya magari yakiwa ni madeni ya mwaka wa fedha 2014/15 hadi 2016/17," alisema.

Aidha, alisema madeni ya mwaka wa fedha 2012/13, 2013/14 na 2017/18 tayari yameshahakikiwa kinachosubiriwa ni fedha kutoka Hazina kwa ajili ya kuyalipa.

Hata hivyo, alisema madeni ya mwaka wa fedha 2018/19 yameandaliwa yanasubiri wahakiki kutoka Hazina ili kuhakiki madeni hayo na baadaye kulipwa.

"Aidha, serikali itaendelea kulipa madeni ya wazabuni wanaotoa huduma mbalimbali ikiwamo chakula cha wafungwa na matengenezo ya magari kadri fedha itakavyopatikana," alisema.

# Madarasa 1,080 mbioni kukamilika

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo (pichani), amesema serikali inaendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa madarasa 1,080 ili kuondokana na uhaba wa miundombinu hiyo.

Jafo alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Susan Lyimo, ambaye alisema suala la upungufu wa madarasa limekuwa likijirudia mara kwa mara.

"Waziri anasema wana takwimu mwaka juzi wanafunzi 133,000 walifaulu, lakini walishindwa kuchaguliwa kutokana na tatizo la madarasa, na mwaka huu zaidi ya wanafunzi 58,000 wamekosa madarasa licha ya kufaulu mtihani wa darasa la saba," alisema.

Alihoji: "Ni kwa sababu gani kama serikali ina 'projection' na inajua wanafunzi wangapi wanafaulu, kwa nini hawana mpango mahususi wa kutenga bajeti ya ujenzi wa miundombinu ili tatizo hilo kwa kipindi cha miaka mitano liweze kuisha, kwa kuwa bado kuna wanafunzi wamefaulu, lakini wataanza shule mwezi wa tatu (Machi)."

Akijibu swali hilo, Waziri Jafo alisema serikali inafanya kila linalowezekana kuhakikisha wanafunzi wote waliofaulu wanapata fursa ya kuendelea na masomo ya sekondari.

Alisema kwa mwaka huu wanafunzi 759,000 waliofaulu na kutokana na kupanda kwa ufaulu asilimia 92 wamechaguliwa kwa awamu ya kwanza na waliosalia 58,000 tayari wamechaguliwa.



"Kwa sasa kuna kazi kubwa ya umaliziaji wa madarasa 1,080 naomba niwahakikishie Watanzania kuwa ukiona wanafunzi wanafaulu ni mafanikio ya uwekezaji yaliyofanywa na serikali, tushikamane kwa pamoja ufaulu mkubwa iwe ni mafanikio ya uwekezaji huu," alisema.

Awali, katika swali la msingi Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Ruth Mollel, alisema Shule ya Msingi Vikindu katika Wilaya ya Mkuranga ina mikondo miwili ya darasa la kwanza hadi la saba, na mwaka 2019 darasa la kwanza na la pili yalikuwa na wanafunzi 300 kila darasa.

"Je, serikali ina mkakati gani kuhakikisha uwiano wa mwalimu na mwanafunzi wa 1:45 unazingatiwa kwa mujibu wa sera ya elimu ya msingi na je, kwa msongamano huo tunaweza kupata wanafunzi walioelimika na kukidhi malengo ya Tanzania ya viwanda?" Alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Tamisemi, Mwita Waitara, alisema ongezeko la uandikishaji wanafunzi katika Halmashauri ya Mkuranga linatokana na juhudi za serikali za kuhamasisha wananchi kuandikisha wanafunzi shuleni kupitia mpango wa eimu msingi bila malipo.

"Ili kukabiliana na msongamano wa wanafunzi katika Shule ya Msingi Vikindu, serikali imechukua hatua mbalimbali ikiwamo kujenga vituo shikizi vya juhudi, Kitangwi, Mitawa na Muungano, kituo shikizi cha Muungano kilichopo katika Kijiji cha Vikindu kinatarajiwa kukamilika mwezi Februari, 2020 na kitakuwa na uwezo wa kupokea wanafunzi 300," alisema.

Alieleza kuwa mkakati mwingine ni wanafunzi kusoma kwa kupokezana ambapo kuna madarasa ya asubuhi na ya mchana.

"Hatua mbalimbali zimechukuliwa na zinaendela kuchukuliwa na serikali ili kuhakikisha msongamano wa wanafunzi darasani unapungua na kuwezesha kupata elimu bora," alisema.



## HABARI ARUSHA

## OPEC yaahidi kusaidia maskini

**Na Allan Isack, ARUSHA**

UMOJA wa nchi zinazouza mafuta duniani (OPEC), unaofadhili miradi ya mpango wa kunusuru kaya maskini, umeahidi kuendelea kufanya kazi na serikali baada ya kuridhishwa na utekelezaji wa miradi inayoifadhili.

Akizungumza mwishoni mwa wiki wakati wa kukagua mradi wa ujenzi wa miundombinu ya Shule ya Sekondari Oldonyowas, Ofisa Mwandamizi wa OPEC, Sharagim Shams, alisema ameridhishwa na utekelezaji huo.

Miradi hiyo inatekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) katika Halmashauri ya Arusha Wilaya ya Arumeru.

"Nimeridhishwa na utekelezaji wa miradi tunayoifadhili nimeshuhudia namna inavyotekelezwa kwa ubora na matumaini yetu itawanufaisha walengwa. Tutaendelea kufanya kazi na serikali ya Tanzania," alisema.

Shams aliwataka walengwa wa miradi ya Tasaf kuitumia vizuri ili kuondokana na umaskini na kuwasaidia kuwapeleka shule watoto wao.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Oldonyowas, Geophray Ayao, alisema ujenzi wa Shule ya Oldonyowas, umeleta mwanga kwa watoto wa eneo hilo na utawezesha kutimiza ndoto walizonazo.

"Awali, watoto walitembea umbali mrefu kwenda kusoma Shule ya Sekondari Oldonyosambu, shule ambayo ipo zaidi ya kilomita 12, umbali huu uliwakatisha tamaa wanafunzi wengi waliacha shule, sambamba na kushuka kwa ufaulu kwenye eneo hili," alisema.

Alisema ujenzi huo umepunguza tatizo la vyumba vya madarasa, nyumba za walimu, mabweni ya wanafunzi pamoja na matundu ya vyoo katika Shule ya Sekondari Oldonyowas.

Mkurugenzi Mtendaji wa Tasaf, Ladislaus Mwamanga, amewapongeza wananchi wa kijiji cha Oldonyowas kwa kuitikia wito wa serikali wa kushiriki katika miradi ya maendeleo.

Mwamanga ameishukuru serikali kwa kuruhusu utekelezaji wa sehemu ya pili ya mpango wa kunusuru kaya maskini kupitia mfuko huo.

Naye Mkuu wa Shule ya Sekondari Odonyowas, Richard Mugyabuso, ameishukuru OPEC, kupitia Tasaf kwa kujenga miundombinu ya shule ikiwamo vyumba vya madarasa, jengo la utawala, matundu ya vyoo pamoja na ujenzi wa mabweni mawili, unaoendelea shuleni hapo kwa ajili ya wanafunzi wa kike 96.

Mratibu wa Tasaf, Halmashauri ya Arusha, Grace Makema, alisema ujenzi wa mradi huo unagharimu Sh. milioni 436.3 ambapo kati ya fedha hizo, Sh. milioni 104.5 zimetumika kujenga jengo la utawala.

Alisema Sh. milioni 79.8 zimetumika kujenga vyumba viwili vya madarasa, ofisi ya walimu na matundu manne ya vyoo, Sh. milioni 76.9 zimejenga nyumba ya walimu zenye sehemu mbili na Sh. milioni 175.1 ni kwa ajili ya mabweni mawili.

Alisema Tasaf ilitoa Sh. milioni 384 na jamii ilichangia kiasi cha Sh. milioni 52.2 sawa na asilimia 12.

# Mtoto wa miaka 11 aeleza mazito alivyotumikishwa miaka 6 misituni

**Na Jaliwason Jasson, MANYARA**

MTOTO wa kiume wa umri wa miaka 11 (jina limehifadhiwa) kutoka kijiji cha Gidewari, Halmashauri ya Hanan'g mkoani Manyara asimulia namna alivyotoroshwa na kutumikishwa kuchunga ng'ombe msituni akiwa na miaka sita.

Akisimulia mkasa huo, mtoto huyo aliiambia Nipashe kuwa, alitoroshwa nyumbani kwao miaka mitano iliyopita akiwa na umri wa miaka sita na kupelekwa msituni alikokabidhiwa ng'ombe zaidi 1,500 ili awachunge.

Akiwa katika Ofisi ya Ustawi wa Jamii wa Halmashauri ya Hanan'g baada ya kupatikana mwezi uliopita, mtoto huyo alisema kuwa kwa kipindi chote alikuwa akichunga mifugo hiyo katika msitu mnene wenye wanyama wakali wakiwamo simba.

Alisema kabla ya kuondoka kwa wazazi wake alirubuniwa na mtu na alitoroka nyumbani kwao kwa lengo la kwenda kufanya kazi ili apate fedha nyingi.

Alisema alivyotoroshwa alipelekwa Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma na kuanza kazi hiyo ya kuchunga mifugo kwenye misitu kwa ujira wa Sh. 10,000 kwa mwezi.

Alisema licha ya yeye kufanya kazi katika mazingira magumu na hatarishi lakini fedha ambazo alitakiwa kulipwa, alikuwa akipatiwa baba yake mzazi ambaye anayeishi Tunduru.

"Baba yangu ambaye alishatengana na mama yangu ndiye alikuwa akipokea malipo hayo, nilikuwa nachunga ng'ombe zaidi 1,500 pekee yangu na nilikuwa nakutana na simba na wanyama wengine wakali.

"Nilikuwa nikiona mnyama mkali najificha katikati ya ng'ombe ili simba asinidhuru. Mvua ikinyesha nilikuwa nakaa chini ya ng'ombe."

Mtoto huyo alisema ng'ombe hao walikuwa wanamilikiwa na watu tofauti ambao amewataja na idadi ya mfuko katika mabano, Edward Gityenga (200), Said Gityenga (300), Daudi Gityenga (100) na mmoja aliyemtambua kwa jina moja la Dk. Gityenga (900).

"Nilikuwa natumikishwa na kuteswa na wafugaji hawa na ilifikia hatua wakanibambikia kesi ambayo nashukuru serikali kupitia Ofisa wa Ustawi wa Jamii wa Wilaya ya Tunduru ambaye ndiye alinisaidia nikarejeshwa nyumbani," alisema.

Akizungumza na gazeti hili kwa njia ya simu, Ofisa Ustawi wa Jamii Wilaya ya Tunduru, Blandina Sekela, alikiri kumfahamu mtoto huyo ambaye alimsaidia kumtoa katika mazingira hayo hatarishi.

Sekela alisema kuwa alikutana na mtoto huyo mahakama ya watoto akiwa na kesi ya kuiba ng'ombe wawili na wakati huo alikuwa tayari amekiri kosa.

"Nilimwomba hakimu mtoto huyu apelekewe hospitali kwanza maana alikuwa anakojoa damu na anatokwa na damu puani na alikutwa pia ana malaria," alisema.

Alisema walifungua kesi na jitihada za kuwatafuta watuhumiwa zilifanyika bila mafanikio hivyo walimsafirisha mtoto kwenda kwao.

Ofisa Ustawi wa Jamii wa Halmashauri ya Hanan'g, Martha Sulle, ambaye alimpokea mtoto huyo alisema anaendelea vizuri ila aliporudi nyumbani kwao baadaye aliogopa kuishi huko hivyo ametafutiwa mahali pa kuishi.

"Mtoto huyu hajawahi kusoma hivyo niliagizwa na Mkuu wa Wilaya nimtafutie shule na tayari atakwenda shule binafsi ya Mountain Hanan'g, tunaomba wadau wajitokeze kumsaidia kumlipia ada," alisema.



Msichana Rawan Dakik mwenye umri wa miaka 18 (kushoto), akijadiliana jambo na Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Mawasiliano wa Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa), Pascal Shelutete (kulia) na Kamishna Msaidizi wa Hifadhi na Maendeleo ya Biashara, William Mwakilema, jijini Arusha juzi. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Mganga Mkuu wa Jiji awaonya wasambaza uvumi homa corona

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

MGANGA Mkuu wa Halmashauri ya Jiji la Arusha, Dk. Simon Chacha, ameonya wananchi wa jiji hilo, kuacha kusambaza taarifa za uwongo za kuwapo kwa raia wa China mwenye virusi vya ugonjwa wa corona.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapo, Dk. Chacha alisema taarifa zinazosambaa kwenye mitandao ya kijamii kuwa kuna raia huyo mwenye virusi hivyo sio za kweli.

"Chanzo cha uvumi huo wanadai kuna raia huyu (jina tunalo) mwenye umri wa miaka 33 tangu ameingia nchini anasiku 15 na kati ya hizo siku mbili alikaa jijini Dar es Salaam, na alipofika Dar es Salaam alipimwa afya yake na hakua na dalili wala homa ya virusi hivyo," alisema.

Alisema baada ya kusambaa kwa taarifa hizo timu ya ufuatiliaji ya magonjwa ya mlipuko, ilimfuatilia mgeni huyo na kubaini alikuja Arusha Januari 15, na alipimwa hakuwa na shida yoyote.

Dk. Chacha aliwaomba wananchi kutosambaza taarifa ambazo hazijathibitishwa na mamlaka husika kwa sababu zinaathari kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Dk. Chacha alitaja dalili za ugonjwa huo kuwa ni mafua, kikohozi, homa kali, kichwa kuuma, kupumua kwa shida na mwili kuchoka.

Mlipuko wa ugonjwa huo wa corona umeripotiwa kutokea Jiji la Wuhan nchini China na hadi jana jumla ya watu waliopoteza maisha walikuwa ni 80 na zaidi ya 2,000 wakiwa wameambukizwa.

Tangu kugundulika kwa ugonjwa huo, mamlaka ya China imesitisha safari za ndege kwa raia wake wanaotoka na kuingia nchini humo.

Juzi, serikali kupitia Waziri wa Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, aliwataka wananchi kuwa watulivu kuhusu mlipuko huo wa homa ya corona na kwamba hakukuwa na Mtanzania yoyote aliyeathiriwa.



HABARI KILIMANJARO

# Benki ya Kilimo yatakiwa kufika vijijini

**Na Mary Mosha, MOSHI**

BENKI ya Maendeleo ya Kilimo nchini (TADB) imeshauriwa kuhakikisha inafikisha huduma zake maeneo ya vijijini ili wakulima waweze kunufaika nayo pamoja na kukuza uchumi wa viwanda kupitia mazao ya kimkakati.

Hayo yalibainishwa na Mwenyekiti wa Chama cha Wenye Viwanda, Biashara na Kilimo (TCCIA) wilayani Moshi, Louis Mbuya na kueleza kuwa benki hiyo ikisogeza huduma yake vijijini wakulima wengi wataweza kulima kwa tija na kuwa na uhakika wa mavuno ambayo ni malighafi tosha kwa viwanda vya ndani na nje ya nchi.

“Ili kutimiza azima ya serikali ya uchumi wa viwanda ipo haja ya wakulima kuongezewa elimu pamoja na rasilimali fedha kwa ajili ya manunuzi ya pembejeo na viuatilifu vitakavyoweza kuleta matokeo chanya katika sekta ya kilimo na uchumi wa viwanda,” alisema Mbuya.

Alisema miaka ya nyuma wakulima wa kahawa walikuwa wakinufaika na Chama Kikuu cha Ushirika (KNCU) kwa kupewa pembejeo, lakini siku hizi hawatoi hivyo benki ya wakulima ndio itabaki kuwa mkombozi.

“Watu kama wakulima wa kahawa wanahitaji dawa nyingi na ukikopa katika benki za kibiashara hauwezi kumudu, gharama ni kubwa kwa kuwa serikali ilituanzishia benki hiyo ndio msaada wetu,” alisema Mbuya.

Aliongeza kuwa kama TADB itajisogeza kwa wakulima, viwanda vingi vitakavyoanzishwa vitakuwa na uhakika wa kupata malighafi ndani ya nchi kutokana na wakulima wengi kulima kisasa hivyo kuwa na uhakika wa mazao.

# Tanapa yabariki Mlima Kilimanjaro kutangazwa kimataifa

**Na Mary Mosha, KILIMANJARO**

SHIRIKA la Hifadhi za Taifa (Tanapa), limeridhishwa na uamuzi wa Mtanzania, Rawan Dakin kwenda kuutangaza Mlima Kilimanjaro katika nchi za Nepal na China.

Dakin (18), aliyejijengea umaarufu akiwa ni Mtanzania mdogo kupanda Mlima Kilimanjaro zaidi ya mara tatu na kufika kilele cha Uhuru chenye urefu wa mita 5,895.

Ofisa Uhusiano wa Tanapa, Paschal Shelutete, alisema tayari Dakin ameanza mazoezi kwa ajili ya kupanda Mlima Everest, Machi mwaka huu.

Kwa mujibu wa Shelutete, Dakin amealikwa kuungana na wapanda mlima wengine maarufu duniani, kupanda Mlima Everest ambao ni mrefu kuliko yote duniani ukiwa na urefu wa mita 8,848.

Wakati Mtanzania huyo akitumia uzalendo wake kuitangaza Tanzania kiutalii, mwaka jana Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamisi Kigwangalla, alisema serikali Tanzania ina mpango pia wa kuanzisha matumizi ya kiberenge kwa ajili ya kuvutia utalii, kwa kuwa hauna madhara.

Alisema wapo watalii watakaopanda mlima huo kwa kutumia njia ya miguu na wapo watakaopanda kwa kutumia kiberenge na kwamba utalii wa kiberenge unatumika katika nchi mbali mbali ulimwenguni.

Alisema faida za kupanda mlima huo kwa kutumia kiberenge ni kubwa kwani utawazesha watalii wengi kupanda Mlima Kilimanjaro kwa wakati mmoja na watalii wazee, watoto na watu wenye ulemavu wataweza kupanda mlima huo.

“Kuna kundi kubwa la watalii wazee ambao hawawezi kupanda mlima kutokana na umri wao, lakini hawa wataweza kuja kupanda mlima Kilimanjaro endapo kutakuwapo na huduma ya kiberenge,” alisema Dk. Kigwangalla.

Alisema kiberenge pia kinaweza kutumika kufanya uokozi wa watalii wanaoshindwa kupanda mlima huo kutokana na sababu mbalimbali za kimazingira na afya.

Alisema utalii ni chimbiko la uhakika wa mapato ya serikali na kutoa wito kwa Watanzania kupenda uzalendo kwa Taifa lao na kutembelea hifadhi za taifa ili kuweza kuimarisha mapato ya nchi.

Tanzania inataka kuongeza idadi ya watalii kupitia magari ya kutumia nyaya katika Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro ambao ndio mlima mrefu zaidi barani Afrika uliosimama.

Alisema tayari serikali imeanza mazungumzo na kampuni moja ya China na nyingine ya Magharibi.

Njia iliyokuwa inapendekezwa kutumika kwa kiberenge hicho cha utalii ni ile ya Machame ambayo kwa mujibu wa watoa huduma, ndio njia inayotumika na wageni zaidi kuliko njia nyingine zote kuelekea mlimani.

Kiberenge hicho kinatajwa kwamba kinaweza kuongeza idadi ya watalii kwa asilimia 50, kwa sababu kina uwezo wa kuwawezesha wale wasioweza kupanda mlima huo kwa miguu kufika kilele cha Uhuru chenye urefu wa mita 5,895.

Aina hiyo ya kuchochea utalii haitakuwa ya mara ya kwanza duniani, kwa vile magari ya kutumia nyaya au viberenge yapo nchini Sweden, Italy na Himalayas.



Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, akizungumza na waandishi wa habari wa mkoa wa Kilimanjaro hivi karibuni, kuhusu namna ya kutatua changamoto zinawazowakabili wanataaluma hao. **PICHA: JAMES LANKA**

# Wafugaji waomba kupatiwa ng’ombe wa maziwa

**Na Mary Mosha, MOSHI**

BAADHI ya wafugaji mkoani Kilimanjaro, wameiomba serikali kuangalia uwezekano wa kuwasaidia ili waweze kupata ng’ombe bora wa maziwa kwa bei nafuu kutoka kwenye mashamba darasa ya serikali.

Wamesema kwa kutimiziwa hitaji hilo kutaongeza upatikanaji na unywaji wa maziwa na kujiongezea kipato.

Wakizungunza na Nipashe wafugaji ho walieleza kuwa wamekuwa wakishindwa kununua ng’ombe bora kutokana na kuwa na kipato kidogo.

Elisa Mkoni mmoja wa wafugaji mkazi wa Machame Wilaya ya Hai, alisema wamekuwa wakikabiliwa na bei kubwa ya ng’ombe aina ya mitamba kutoka kwa mashirika na watu binafsi hali ambayo anashindwa kununua na kumlazimu kuendelea kufuga ng’ombe wa kienyeji wanaotoa maziwa kidogo.

“Zipo aina mbalimbali za ng’ombe bora wa maziwa yaani Friesien, Aryshire na Jersey wanauwezo mkubwa wa kutoa maziwa, lakini wanauzwa kwa gharama kubwa kuanzia Sh. milioni 1.6 hadi milioni mbili katika mashirika yasiyo na kiserikali na watu binasi hali ambayo inatufanya tushindwe kumudu kuwahudumia kwa faida katika kujiingizia kipato na kuongeza maziwa katika soko,” alisema Mkoni na kuongeza:

Kwa upande wake mtaalamu wa sekta ya maziwa kutoka Shirika la Uholanzi SNV, Benovila Balama, alisema licha ya wafugaji kuiomba serikali kuangalia uwezekano wa kupunguza bei ya ng’ombe wa maziwa lakini utafiti unaonyesha ng’ombe waliopo mkoani Kilimanjaro wanauwezo mkubwa wa kutoa maziwa lakini wanakabiliwa na changamoto ya malisho.

Alisema wafugaji hawana elimu ya kutosha juu ya namna bora ya kuwalisha ng’ombe na mazingira bora ya ng’ombe kuishi ili kuleta tija katika sekta ya maziwa.

“Serikali ya mkoa ihakikishe inatoa elimu kwa wafugaji juu ya utengenezaji wa mabanda bora ya kulishia ng’ombe, lishe sahihi ili waweze kupata maziwa mengi na kujikwamua kiuchumi kwani maziwa ni chakula na pesa,” alisema Balama.

## Miaka 75 kukombolewa kambi ya mateso Poland



Ukurasa 17



Ukurasa 18


## Kinamama Shinyanga wachechemea serikali mitaa, wapania uchaguzi mkuu


# siasa

JUMATANO JANUARI 29, 2020

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe

Ukurasa 20

## Bunge Marekani linavyokerwa na mipango ya Rais wao Trump

# NEC inavyoshika kasi kudodosa kona zote kuboresha daftari kura

• Machi kuanika ilichofanya mikoa 31

**Na Bartholomew Wandi**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) ni nini? Hicho si chombo kigeni masikioni na machoni mwa umma. Ni sehemu ya maisha yao.

Kimsingi, kinatokana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, ikibeba majukumu mbalimbali, ikiwamo uandikishaji wapiga kura nchini.

Eneo kuu ambako imekasimiwa jukumu la kuratibu na kusimamia uchaguzi unaomhusu Rais, wabunge na madiwani.

Katika utaratibu uliopo, Uboreshaji Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, kisheria hutakiwa kufanyika mara mbili ndani ya miaka mitano, yaani baada ya uchaguzi mmoja kumalizika na kabla ya unaofuata.

Uchaguzi Mkuu wa Rais na Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Madiwani wa Tanzania Bara wa mwaka 2015 umeshamalizika na ndiyo maana Julai 18 mwaka jana, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alialikwa kuzindua uboreshaji Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

**INAENDELEA UK.16**




Wananchi wakiwa kwenye foleni katika kituo cha kuandikisha wapiga kura, wakisubiri zamu zao. **PICHA ZOTE: KWA HISANI YA NEC**

Tpb Bank
Grow with us

# TPB BANK PLC

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA(HESABU AMBAZO HAZIJAKAGULIWA)

metolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

## TPB BANK PLC
### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 DESEMBA, 2019
*Kiasi kwa shilingi milioni*

| | | | Robo Mwaka ya /Mwaka wa sasa 31.12.2019 3 | Robo Mwaka/Mwaka uliopita 30.09.2019 |
|---|---|---|---|---|
| A. | | **MALI** | | |
| | 1 | Fedha Taslimu | 37,749 | 30,297 |
| | 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 25,827 | 10,074 |
| | 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 100,588 | 74,494 |
| | 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 14,675 | 20,105 |
| | 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 3 | 9 |
| | 6 | Miamala Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| | 7 | Bili Zilizoafikiwa | 0 | 0 |
| | 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | 0 | 0 |
| | 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 0 | 0 |
| | 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | 0 | 0 |
| | 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 420,683 | 412,939 |
| | 12 | Mali Nyingine | 23,468 | 22,005 |
| | 13 | Uwekezaji wa Hisa | 0 | 0 |
| | 14 | Akaunti za udhamini | 0 | 0 |
| | 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 17,176 | 17,234 |
| | **16** | **JUMLA YA MALI** | **640,170** | **587,156** |
| B | | **DHIMA** | | |
| | 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | - | - |
| | 18 | Amana za Wateja | 435,444 | 406,590 |
| | 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 0 | 0 |
| | 20 | Amana Maalumu | 0 | 0 |
| | 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 1,096 | 1,004 |
| | 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 0 | 0 |
| | 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 13,997 | 12,925 |
| | 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | 0 | 0 |
| | 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| | 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa | 2,054 | 2,895 |
| | 27 | Dhima Nyingine | 13,082 | 13,431 |
| | 28 | Madeni | 74,719 | 56,239 |
| | **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **540,393** | **493,084** |
| | **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI** ***(16 kutoa 29)*** | **99,777** | **94,072** |
| C. | | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| | 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 28,072 | 28,072 |
| | 32 | Akiba ya Mtaji | - | 0 |
| | 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 44,576 | 43,376 |
| | 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 16,909 | 12,404 |
| | 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 10,220 | 10,220 |
| | 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | 0 | 0 |
| | **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **99,777** | **94,072** |
| | 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 0 | 0 |
| | 39 | Mikopo Chechefu | 25,132 | 25,319 |
| | 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 19,218 | 19,135 |
| | 41 | Mali Nyingine Chechefu | 70 | 55 |
| D. | | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| | (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 15.59% # | 16.02% |
| | (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 5.67% | 5.81% |
| | (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 101.79% | 107.20% |
| | (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 65.71% | 70.33% |
| | (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 82.59% | 83.90% |
| | (vi) | Ongezeko la Amana | 7.10% | 3.35% |
| | (vii) | Ongezeko la Mali | 9.03% | 1.10% |

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI
### KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 31 DESEMBA, 2019
*Kiasi kwa shilingi milioni*

| | Robo ya Mwaka sasa 31-Dec-19 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31-Dec-18 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Dec-19 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31-Dec-18 |
|---|---|---|---|---|
| 1 Mapato ya Riba | 24,717 | 24,381 | 100,178 | 95,945 |
| 2 Gharama za Riba | (6,615) | (4,541) | (22,496) | (17,870) |
| 3 Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2) | **18,102** | **19,840** | **77,683** | **78,075** |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | (374) | (953) | (1100) | (1,265) |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (2,353) | (3,258) | (10,444) | (13,656) |
| 6 **Mapato Yasiyo ya Riba**: | **9,585** | **7,619** | **29,642** | **22,371** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za | 1,195 | 1,004 | 4,491 | 3,492 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 4,297 | 3,204 | 14,772 | 14,867 |
| 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | 4,093 | 3,410 | 10,379 | 4,012 |
| 7 **Gharama Zisizo za Riba:** | **(18,730)** | **(17,864)** | **(71,972)** | **(68,337)** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | 8,178 | 8,153 | 32,799 | 31,280 |
| 7.2 Ada na Kamisheni | 1,486 | 1,788 | 4,354 | 5,493 |
| 7.3 Gharama Nyingine | 9,066 | 7,924 | 34,819 | 31,563 |
| 8 **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **6,230** | **5,384** | **23,809** | **17,188** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | 1,725 | 1,521 | 6,900 | 5,086 |
| 10 **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **4,505** | **3,863** | **16,909** | **12,102** |
| 11 **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | **-** | **-** | **-** | **619** |
| 12 **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **4,505** | **3,863** | **16,909** | **12,721** |
| 13 Idadi ya Waajiriwa | 926 | 888 | 926 | 888 |
| 14 Mapato kwa Hisa | 160 | 77 | 602 | 431 |
| 15 **Idadi ya Matawi** | 38 | 36 | 38 | 36 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.72% | 0.68% | 2.87% | 2.26% |
| (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 4.57% | 4.69% | 18.40% | 15.34% |
| (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 54.60% | 55.83% | 55.44% | 57.76% |
| (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 3.42% | 4.07% | 15.55% | 16.08% |

**Tarakimu za wastani zitakokotolewa kwa kujumlisha salio la mwisho kwa miezi inayohusika katika kipindi na kugawanya kwa idadi ya miezi katika kipindi hicho.**

## TPB BANK PLC
### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA
#### KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 31 DESEMBA, 2019
*Kiasi kwa shilingi milioni*

| | | Robo Mwaka ya sasa 31-Dec-19 | Robo Mwaka iliyopita 30-Sep-19 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Dec-19 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31-Dec-18 |
|---|---|---|---|---|---|
| **I:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za** | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | 6,230 | 6,168 | 23,809 | 17,188 |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | |
| | - Hasara Katika Mali | 4,245 | 5,128 | 8,329 | 7,144 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (7,744) | (10,756) | 9,325 | (90,108) |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | (22) | (149) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 28,855 | 13,171 | 50,354 | 67,572 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi | - | - | - | (5,142) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 4,974 | (5,676) | (2,259) | 9,046 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (1,464) | (2,821) | (1,949) | (889) |
| | - Kodi Iliyolipwa | (1,725) | (1,725) | (6,900) | (6,084) |
| | - Mengineyo (bainisha) | (6,631) | (9,319) | (43,745) | 6,325 |
| | *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji* | 26,740 | (5,829) | 36,942 | 4,905 |
| **II:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za** | | | | |
| | Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (2,511) | (813) | (5,458) | (8,695) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | 1 | 154 |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji* | (2,511) | (813) | (5,457) | (8,540) |
| **III:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | (1,210) | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | 12,000 | 12,000 | 526 |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha | - | *12,000* | *10,790* | *526* |
| **IV:** | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | 24,229 | 5,357 | 42,275 | (3,108) |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | **23,306** | **17,949** | **5,260** | **8,368** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 47,535 | 23,306 | 47,535 | 5,260 |

## TPB BANK PLC
### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA TAREHE 31 DESEMBA, 2019
*Kiasi kwa shilingi milioni*

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **28,072** | **-** | **40,539** | **135** | **3,913** | **10,262** | **82,920** |
| Mabadiliko ya mpito ya IFRS 9 | - | - | - | - | - | - | - |
| Hamisho kwenda hifadhi ya kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Faida ya mwaka | - | - | 16,909 | - | - | - | **16,909** |
| Mapato mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| Hifadhi ya jumla | | - | 3,913 | - | (3,913) | - | **0** |
| Gawio lililolipwa | - | - | (10) | - | - | - | **(10)** |
| Hamisho kwenda/kutoka mapato yaliyohifadhiwa | - | - | 135 | (135) | - | - | - |
| Mengineyo | | | | | | (42) | **(42)** |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **28,072** | **-** | **61,485** | **0** | **0** | **10,220** | **99,777** |
| **Mwaka uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **28,072** | **-** | **28,386** | **288** | **3,101** | **-** | **59,846** |
| Mabadiliko ya mpito ya IFRS 9 | - | - | 1,291 | - | - | - | **1,291** |
| Hamisho kwenda hifadhi ya kisheria | - | - | (1,291) | 1,291 | - | - | - |
| Faida ya mwaka | - | - | 12,102 | - | - | - | **12,102** |
| Mapato mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| Hifadhi ya jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (1,200) | - | - | - | **(1,200)** |
| Hamisho kwenda/kutoka mapato yaliyohifadhiwa | - | - | 632 | (1,444) | 812 | - | - |
| Mengineyo | - | - | 619 | - | - | 10,262 | **10,881** |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **28,072** | **-** | **40,539** | **135** | **3,913** | **10,262** | **82,920** |

UTANGULIZI MWINGINE
Benki ilipata adhabu ya TZS 92,624,849.52 kwa kutokidhi uwiano wa kima cha chini cha cha Ukwasi cha 20% kwa robo ya 4, 2019

Katika kuandaa taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8)

| *Jina na Cheo* | *Saini* | *Tarehe* |
|---|---|---|
| **SABASABA K. MOSHINGI** (Ofisa Mtendaji Mkuu) | IMESAINIWA | **27.01.2020** |
| **REGINA E. SEMAKAFU** (Mkuu wa Fedha) | IMESAINIWA | **27.01.2020** |
| **SOSTHENES F. NYENYEMBE** (Mkaguzi Mkuu wa Ndani) | IMESAINIWA | **27.01.2020** |

Sisi tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi,tunathibitisha usahihi wa Taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathimini taarifa hizi,na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya kimataifa vya uwasilishaji wa Taarifa za fedha na matakwa ya sheria ya Benki na Taasisi za fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi

| | | |
|---|---|---|
| **DR. EDMUND B. MNDOLWA** Mwenyekiti wa Bodi | IMESAINIWA | **27.01.2020** |
| **MR. MACRICE D. MBODO** Mjumbe wa Bodi | IMESAINIWA | **27.01.2020** |

Head Office: LAPF Towers Bagamoyo Roard. P.O. Box 9300 Dar es Salaam Tanzania. Telephone: +255 22 2162940, Fax: +255 22 2114815, Email: info@tpbbank.co.tz

# TANGAZO

## TPB BANK MINIMUM DISCLOSURE OF BANK RATES AND CHARGES

| TYPE OF CHARGE | TRANSACTION / ITEM | CHARGES |
|---|---|---|
| Minimum Opening Balance | Quick Account | 20,000 |
| | Salary Account | FREE |
| | Platinum Account | 15,000 |
| | Call Account | 100,000 |
| | Minor Account | 20,000 |
| | Scout Minor | 10,000 |
| | Scout | 30,000 |
| | WADU | 20,000 |
| | YANGA VIP Card | 1,200,000 |
| | YANGA Member Card | 25,000 |
| | Group Account | FREE |
| Bank Statement | | Within a month is FREE and more than a month is 1,500 per document |
| Monthly Maintenance Fee | Savings Account | 1,300 |
| | Current Account | 6,500 |
| | Platinum Account | 1,300 |
| | WADU Account | FREE |
| | Call Account | 6,500 |
| | Minor Account | FREE |
| | Group Account | FREE |
| Dormant Accounts Fee | 1 year to 5 years | 1,300 |
| | 6 years to 10 years | 5,000 |
| | 11 years to 15 years | 10,000 |
| Activation of Dormant Account | | FREE |
| ATM Charges | ATM Balance Enquiry- All cards | 300 |
| | Mini statement | 300 |
| | Cash Withdraw on TPB ATMs | 1,300 |
| | Cash Withdraw on other UMOJA SWITCH ATM | 1,300 |
| POS Branches | Balance Enquiry | 150 |
| | Mini statement | 150 |
| | Deposit | FREE |
| | Transfer | 650 |
| | POS Withdraw | 2,600 |
| POS Agents | Balance Enquiry | 150 |
| | Mini statement | 150 |
| | Deposit | FREE |
| | Transfer | 650 |
| | POS Withdraw | see Tiered Fees 1 |
| Mobile Banking | Balance Enquiry | 300 |
| | Mini statement | 300 |
| | Full Statement | 400 |
| | Pin Charge | FREE |
| | Notification /Alert | 200 |
| | Account Transfer | 650 |
| | Mobile Agent Deposit | 200 |
| | Mobile Agent Withdraw | see Tiered Fees 2 |
| | Mobile Money to Bank Deposit | 1,300 |
| Closing Account | | 13,000 |
| FDR Min. Opening Balance | | 100,000 |
| ATM Issuance and Replacement Fees | Popote Card | 15,000 |
| | Yanga Member card | 20,000 |

| TYPE OF CHARGE | TRANSACTION / ITEM | CHARGES |
|---|---|---|
| Other ATM & Normal Card | Pin Re-issue | FREE |
| | Collection of ATM crad at Non Domicile Branch | 6,500 |
| | Uncollected and destroyed ATM card | 6,500 |
| | First ID card (Local and Foreign Currency) | 4,000 |
| | Replacement Of ID card | 2,600 |
| Cash withdraw | Teller withdraw upto 10,000,000 | 2,600 |
| | Teller withdraw from 10,000,001 to 50,000,000 | 5,000 |
| | Teller withdraw from 50,000,0001 to 100,000,00 | 15,000 |
| | Teller withdraw above 100,000,001 | 30,000 |
| Cheques Fees | Cheques Clearing Fee | 3,000 |
| | Special Clearance | 50,000 |
| | Dishonoured Cheque | 35,000 |
| Electronic Fund Transfer (EFT) | TISS Inwards | FREE |
| | TISS- Outward | 10,000 |
| Standing Order | Within the Bank | 1,300 |
| | To other Banks | 13,000 |
| POS Withdraw &Money Transfer/ Tiered fees | POS Withdraw | Tiered 1 |
| Tiered 1 | 0-10,000 | 800 |
| | 10,001-50,000 | 1,000 |
| | 50,001-100,000 | 1,300 |
| | 100,001-250,000 | 2600 |
| | 250,001-500,000 | 4,600 |
| Tiered 2 | TPB Mobile Transfer Fee | Tiered 2 |
| | 0-10,000 | 850 |
| | 10,001-50,000 | 1,200 |
| | 50,001-100,000 | 1,500 |
| | 100,001-250,000 | 2,800 |
| | 250,001-500,000 | 4,600 |

### RATES AND CHARGES FOR USD ACCOUNT

| TYPE OF CHARGE | TRANSACTION / ITEM | CHARGES |
|---|---|---|
| Maintenance Fee | Savings Account | 1 |
| | Current Account | 5 |
| Deposit Fee | Non Account Holder | Free |
| Opening Balance | | 50 |
| Account closure fee | | 10 |
| Bank Statements | | Free |
| | Balance Enquiry- Banking Hall | Free |
| | Confirmation letter | Free |
| Withdraw Fees | 0-5,000 | 5 |
| | Above 5,000 | 20 |
| Cheque | Special clearance | 40 |
| | Unpaid cheque- Refer to Drawer | 10 |
| | Stop Payment | 20 |
| Dormant | Dormant Account Fee | 5 |
| | Re- Activation | Free |
| TISS | | 10 |

Tpb Bank Grow with us

+255 787 669 977 tpbbank//facebook tpbbank//instagram www.tpbbank.co.tz

## LENDING INTEREST RATES AND OTHER CHARGES

### 1. FEES ON CONSUMER LOANS

| S/N | CATEGORY | INTEREST RATE/ CHARGE RATE |
|---|---|---|
| 1. | Consumer Loan Administration Fee | 1.5% of the Approved Loan. Minimum TZS. 10,000/= |

### 2. FEES ON WASTAAFU LOANS

| S/N | CATEGORY | INTEREST RATE/ CHARGE RATE |
|---|---|---|
| 2. | Loan Application Fee | TZS. 10,000/= |
| 3. | Loan Administration Fee | 1.5% Minimum. TZS. 10,000/= Maximum TZS. 100,000/= |

### 3. OTHER CHARGES ON INDIVIDUAL MICRO CREDIT

| S/N | CATEGORY | INTEREST RATE/ CHARGE RATE |
|---|---|---|
| 1. | MIC Loan Application Fee | TZS. 20,000/= |
| 2. | MIC Loan Processing/Administration Fee | 1.5% Minimum TZS. 50,000/= |

### 4. INTEREST RATES AND OTHER CHARGES ON BUSINESS LOANS

| S/N | CATEGORY | INTEREST RATE/ CHARGE RATE |
|---|---|---|
| 1. | Loan Application Fees for Business and Personal Loans | TZS. 50,000/= |
| 2. | Loan Administration Fee - Business and Personal loans | 1.5% of the Approved Amount |



# NEC inavyoshika kasi kudodosa kona zote kuboresha daftari kura



Wananchi wakiwa kwenye foleni katika kituo cha kuandikisha wapiga kura, wakisubiri zamu zao kuingia ndani wajiandikishe au kuboresha taarifa zao katika maeneo tofauti nchini. **PICHA ZOTE: KWA HISANI YA NEC.**

**INATOKA UK.13**

Hiyo ni inayohusu mikoa 31 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa awamu ya kwanza. Uzinduzi ulifanyika mkoani Kilimanjaro na kazi hiyo iliendelea hadi sasa imetimu mikoa mingine 27, daftari limeshaboreshwa.

Rekodi ya NEC inataja mikoa iliyomaliza Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kuwa ni: Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Simiyu, Mara, Mwanza, Shinyanga na Geita.

Mingine inatajwa kuwa ni Kagera, Kigoma, Tabora, Katavi, Rukwa, Songwe, Singida, Dodoma, Mbeya, Iringa, Njombe na Ruvuma, Lindi na Mtwara,.

Kwa upande wa visiwani imajumuisha mikoa ya: Mjini Magharibi, Kaskazini Unguja, KusiniUnguja, Kaskazini Pemba na Kusini Pemba,

Mikoa minne iliyobaki kuboresha daftari hilo, Tanga, Morogoro, Pwani na Dar es Salaam, inaelezwa mchakato unaendelea kufanikisha.

Hadi sasa tathmini zinaonyesha kuwapo kasi kubwa ya uboreshaji Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kulinganana malengo na changamoto zilizokuwapo, ikiwamo kupisha majukumu mengine nyeti ya kitaifa kama; Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, mitihani ya kitaifa darasa la saba, kidato cha pili na cha nne.

> Mikoa minne iliyobaki kuboresha daftari hilo, Tanga, Morogoro, Pwani na Dar es Salaam, inaelezwa mchakato unaendelea kufanikisha.

Kwa mujibu wa mikakati na ratiba ya tume ilyopo, ukamilishaji kazi ya kuboresha daftari katika mikoa minne iliyobaki, inatazamiwa kumalizika mwezi ujao.

Utaratibu ulivyo, awamu ya kwanza ya kazi hiyo itakamilika pale Daftari la Awali la Wapiga Kura litakapowekwa wazi huko kwenye ofisi za kata, mnamo Machi mwaka huu, ili wapiga kura walioandikishwa upya na waliboresha taarifa au kuhamisha taarifa waziangalie.

Hiyo, ni katika mtazamo wa ukaguzi kuona kama taarifa ziko sahihi hazijakosewa na zenye kasoro kuwekewa pingamizi, kwa ajili ya hatua nyinginezo za kisheria.

### SIFA VS HAKUNA SIFA

Watu wasio na sifa ambao waliandikishwa kuwa wapiga kura Wapya kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, ni ambao si raia au wenye uraia wa nchi mbili; wana utii wa nchi nyingine; wamethibitishwa na daktari hawana akili timamu; na wamehukumiwa na mahakama adhabu ya kifo.

Sababu nyingine za kukosesha sifa, ni wapiga kura wanaotumikia kifungo cha zaidi ya miezi sita gerezani, wamezuiliwa kujiandikisha kupiga kura kwa sheria nyinginezo kwa makosa yanayohusiana na uchaguzi.

Pia, kwa walioko hadi siku ya kupigwa kura, hawatakuwa katika umri unaoruhusiwa kupiga kura kisheria ifikapo siku ya uchaguzi, watakosa sifa ya kuandikishwa.

Watu ambao wana sifa za kuandikishwa kuwa wapiga kura wapya kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, ni wale ambao ni raia wa Tanzania, wametimiza umri wa miaka 18.

Pia, nafasi hiyo inawaangukia wapiga kura ambao watatimiza umri wa miaka 18 ifikapo siku ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 na hawajapoteza sifa kwa mujibu wa sheria za uchaguzi au nyingine yoyote iliyotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa ujumla, litawahusu wote wenu sifa walitimiza miaka 18 na kuendelea ambao hawakuandikishwa mwaka 2015 na watakaotimiza umri unaotakiwa Oktoba 18, mwaka huu.

Pia, wanaoangukia kundi hilo ni waliojiandikisha mwaka 2015 na sasa wamehama kata na jimbo moja kwenda lingine na kuondoa waliokosa sifa kama kufariki dunia au kupata uraia wa nchi nyingine.

Wengine katika orodha hiyo ni ambao jinsia zao, tarehe za kuzaliwa na majina yalikosewa wakati wa uandikishaji wa mwaka 2015 na waliopoteza kadi zao au kadi zao za kupigia kura ziliharibika.




### WASIOHITAJIKA KUANDIKISHWA

Kwa walioandikishwa mwaka 2015 na wana kadi ambazo hazijakosewa taarifa zao, hazijafutika maandishi au picha na hawajahama Kata au jimbo kwenda katika kata au Jimbo lingine la uchaguzi, hawahitaji kwenda vituoni kupata kadi nyingine.

Hao wana wajibu wa kuendelea kuzitunza kusubiri uchaguzi mkuu na nyingineo ndogo zitakazotokea, baada ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba ijayo kupita.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi, inatumia njia mbalimbali kuwahimiza na kuwahamasisha wananchi wote wanaohusika na zoezi hili la uboreshaji waende vituoni wakajiandikishe na kuboresha taarifa zao, ili waweze kushiriki Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020.

Njia ambazo NEC inatumia kuwahimiza na kuwahamasisha wananchi waende vituoni, ni matangazo kupitia vyombo vya habari, kama radio, televisheni, vipindi mubashara kwenye radio, mahsusi kuboresha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

> Kwa upande wa visiwani imajumuisha Mjini Magharibi, Kaskazini Unguja, KusiniUnguja, Kaskazini Pemba na Kusini Pemba.

Mengine yanatajwa ni gari la matangazo la halmashauri husika, matangazo ya asasi za kiraia, kushiriki maonyesho mbalimbali ya kitaifa kama Sabasaba, Nanenane, mikusanyiko ya kijamii kama sokoni, minadani, kwenye tamasha na mitandao ya kijamii.

Hivi sasa rai ya NEC, ni Kila mwenye sifa ya kuandikishwa kuwa wapiga kura, aende kituoni kujiandikisha, ili kuboresha taarifa zake chini ya msukumo wa kivuli cha usemi wa Tume 'Kadi yako kura yako, nenda kajiandikishe.

***Mwandishi wa makala hii ni Ofisa Habari Mkuu wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi na anapatikana kwa simu: (+255) 0754 203015.***

## Miaka 75 kukombolewa kambi ya mateso Poland



Wazee walioteswa katika kambi hiyo katika zama za utoto wao, wakiweka mashada ya maua kukumbuka wenzao waliokufa. **PICHA: MTANDAO**

WATU walionusurika kifo kwenye kambi ya mateso ya Auschwitz, wamekutana tena kwenye kambi hiyo nchini Poland tangu ilipokombolewa miaka 75 iliyopita.

Watu hao waliozeeka kiumri, waliweka maua kando ya ukuta wa kambi ambako wafungwa wengi waliuawa wakati wa vita vikuu vya pili.

Viongozi kutoka nchi mbalimbali wanatarajiwa kujiunga na wazee hao kwa ajili ya kukumbuka kukombolewa kambi ya Auschwitz na majeshi ya kisoviet miaka 75 iliyopita.

Hata hivyo, hafla hiyo inafanyika katika muktadha wa wasiwasi juu ya kujitokeza tena kwa chuki dhidi ya Wayahudi duniani kote. Ujerumani pia jana imekumbuka ukombozi wa kambi hiyo ya mauaji kwa kufanyika shughuli mbalimbali.

Rais wa Ujerumani, Frank - Walter Steinmeier, alikutana na watu watatu walionusurika kwenye kambi hiyo kwa ajili ya mazungumzo, Hermann Höllenreiter, Peter Gardosch na Pavel Tussig waliokuwa wageni wa heshima kwenye kasri la rais la Bellevue mjini Berlin.

Wazee hao wote walipelekwa kwenye kambi ya Auschwitz wakiwa watoto na baada ya mkutano huo wa Rais Steinmeier, aliandamana na wahanga kwenda kwenye kambi ya Auschwitz-Birkenau.

Kiongozi wa Ujerumani, Frank-Walter Steinmeier, alitarajiwa kuweka shada la maua na kushiriki katika shughuli mbalimbali za kumbukumbu juu ya mauaji hayo ya halaiki yaliyofanywa na manazi wa Ujerumani ambapo maelfu ya Wayahudi waliuliwa.

Watu zaidi ya milioni moja waliuawa, idadi kubwa wakiwa ni Wayahudi. Baadaye, Kansela wa Ujerumani, Angela Merkel na Waziri Mkuu wa Poland, Mateusz Morawiecki, walitarajiwa kufungua tamasha la kuchangisha fedha zitakazokabidhiwa kwa wakfu wa Auschwitz-Birkenau.

Ujerumani inakumbuka miaka 75 tangu kukombolewa kwa kambi hiyo, huku kukiwa na wasiwasi juu ya kuongezeka tena kwa chuki dhidi ya Wayahudi nchini Ujerumani.

Waziri wa Mambo ya nje Heiko Maas, amewaambia waandishi habari mjini Berlin kwamba, Ujerumani italiweka suala la kupambana na chuki dhidi ya wayahudi kuwa muhimu sana katika ajenda yake ya kisiasa, wakati nchi hiyo inajitayarisha kushika usukani wa kuongoza shughuli za Umoja wa Ulaya (EU) kwa muda wa nusu mwaka, pia Rais wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa,baadae mwaka huu.

Watu zaidi ya milioni 25 wameshaitembelea kambi ya Auschwitz tangu mwaka 1947 nchini Poland na sasa kila mwaka watu zaidi ya milioni mbili kutoka duniani kote wanaitembelea sehemu hiyo iliyoko kusini mwa Poland. **DW**

UCHAGUZI WA VIONGOZI...

# Kinamama Shinyanga wacheche serikali mitaa, wapania uchaguz

## • RC: Kila atakayejitosa 'nitambeba' • DC: Mwenzer nimefanikiwa hivi • Wenyewe wahamasika na kuji

**Na Marco Maduhu,** Shinyanga

KUWAPO mitazamo hasi kutoka mila na desturi kandamizi, ni sababu zinazozaa vikwazo kwa wanawake kushindwa kushiriki kugombea nafasi za uongozi.

Kutokana na hali hiyo, imesababisha kuwapo idadi ndogo ya wanawake katika fursa za uongozi nchini na hata nchi nyinginezo duniani na hadi sasa Katiba ya nchi inaelekeza utoaji haki sawa, ikiwamo ya uongozi pasipo kubaguana.

Mtandao wa kijinsia Tanzania (TGNP), mwaka jana ulizindua Kitabu cha Ilani ya Uchaguzi kwa Wanawake, kikiwahamasisha wajitokeze kwa wingi kugombea nafasi hizo, iwe uongozi wa serikali ya mtaa ambayo uchaguzi wake ulifanyika mwaka jana na uchaguzi mkuu, utakaofanyika mwaka huu.

**KULIVYO SHINYANGA**

Wanawake mkoani Shinyanga, ni waathirika wakuu wa mila kandamizi na kufikia hatua ya kuogopa kujitokeza kugombea nafasi za uongozi kwenye kipindi cha uchaguzi na kusababisha kuwapo mwitikio mdogo wa kinamama kugombea uongozi.

Matokeo ya uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka jana katika Manispaa ya Shinyanga, nafasi ya uenyekiti wa kijiji ambayo kuna vijiji 17, hakuna mwanamke aliyeshinda nafasi hiyo.

Pia, katika nafasi ya uongozi wa mitaa 55, wanaume 49 na wanawake walikuwa sita. Pia, katika vitongoji 84, kuna wanaume 76 na wanawake nane.

**WANASIASA**

Habiba Ramadhani, ni Mwenyekiti wa Mtaa wa Kitangili Manispaa ya Shinyanga, aliyeshinda nafasi hiyo katika awamu ya pili sasa.

Mama huyo tangu mwaka 2014 alipoanza kuwania nafasi hiyo hadi 2019 ameshinda tena kiti hicho na anasema wanawake wanaopewa nafasi wana uwezo wa kuongoza jamii. Anarejea mwaka 2014, kwamba mwanamke aliyejitokeza nafasi ya uenyekiti wa Mtaa wa Kitangili, alikoshindana na wanaume wanne, akijigamba kwamba, kujiamini kwake na kujipangilia vizuri kisera, aliwashinda wanaume hao.

"Baada ya kupata uongozi wa uenyekiti wa mtaa huu wa Kitangili, nikaona nafasi hii nisiichezee, bali nijitume kufanya kazi kuionyesha jamii kuwa wanawake tunaweza kuongoza kuliko hata wanaume.

"Nikaanza kushughulika tu na kutatua matatizo ndani ya jamii pamoja na kuwa nao karibu muda wote,"anasema Ramadhani.

"Kazi hii ya uenyekiti wa mtaa, ni ngumu kwa sababu haina hata mshahara na watu wana matatizo mengi huku wengine wanakuja kunililia njaa.

" Lakini, sisi wanawake, viongozi huwa tuha huruma sana, hasa pale unapoangalia watoto wa familia ambayo haina chakula, ina nibidi nitoe chakula ndani na kugawana nao kidogo," anafafanua.

"Katika awamu yangu ya uongozi mwaka 2014, nimetatua kero nyingi sana za wananchi, ikiwamo migogoro ya ardhi, familia," anasema na anataja miradi mingine anayoitekeleza ni kuchonga barabara ngumu kilomita tatu na ya kawaida kilomita 2.5 na kuweka karavati moja.

Anataja mengine anayoshiriki kutekeleza, ni kuvuta umeme na mradi wa maji, kuwa mambo yaliyofamnya achaguliwe tena kuongoza Mtaa wa Kitangili, hata akachaguliwa tena mwaka 2019 kwa awamu ya pili.

Kwa mujibu wa Habiba, baada ya kushuhudia kukubalika kwake kisiasa na kiutendaji, sasa ananuia kuwania nafasi ya udiwani katika Kata ya Kitangili.

Diwani wa Kata ya Kolandoto, katika Manispaa ya Shinyanga, Agnes Machiya, aliyekwishawahi kuwa Naibu Meya wa Manispaa, anataja siri ya mafanikio yake akiwa mwanamke kiongozi, ni uchapaji kazi, kutatua kero za wananchi na kuwatekelezea miradi ya maendeleo.

"Mwaka (2005 hadi 2010) nilikuwa diwani wa viti maalumu na baada ya kuonekana na kubadilika na wananchi, ikabidi mwaka 2010 nijitose kugombea nafasi ya udiwani kwenye kata ya Kolandoto.

"Nikifanikiwa kushinda na sasa ni awamu yangu ya pili naongoza na kwenye uchaguzi mkuu mwaka huu nagombea tena," anasema Machiya.

"Mimi ni diwani pekee mwanamke Manispaa ya Shinyanga ambaye namiliki kata (wa kuchaguliwa). Hivyo, naomba madiwani wenzangu wale wa viti maalum ambao wana uzoefu tayari wa uongozi, kwenye uchaguzi mkuu wa



Kamishna wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Balozi Omari Ramadhani Mapuri (mwenye nguo nyeusi kageuza mgongo), alipofungua mkutano wa Tume na Wadau wa Uchaguzi mkoani Shinyanga, mwaka jana. **PICHA: MTANDAO.**

> "Nikifanikiwa kushinda na sasa ni awamu yangu ya pili naongoza na kwenye uchaguzi mkuu mwaka huu nagombea tena.



Mwenyekiti wa chama cha ACT-Wazalendo Mkoani Shinyanga, Siri Yasini. **PICHA ZOTE: MARCO MADUHU.**

# emea
# zi mkuu

## nu
## ipanga





Mkuu wa Mkoa Shinyanga, Zainab Telack. **PICHA: MAKTABA.**



Mwenyekiti wa Mtaa wa Kitangili, katika Manispaa ya Shinyanga, Habiba Ramadhani, akielezea siri ya mafanikio yake katika uongozi, akishinda mara mbili katika uchaguzi serikali ya mtaa.

mwaka huu, wajitokeze kugombea udiwani kwenye kata ili tuwe na uwiano sawa na wanaume," anasema.

### KIONGOZI CHAMA

Siri Yasini ni Mwenyekiti wa chama cha ACT-Wazalendo Mkoani Shinyanga, anaainisha nafasi za uongozi aliyokwishawahi kuzishika kama mwanamke kiongozi.

Anaanzisha historia yake, kwamba mwaka 1999 alikuwa Mjumbe wa Serikali ya Mtaa wa Chamaguha katika Manispaa ya Shinyanga na mwaka 2000 hadi 2005, alikuwa Mwenyekiti wa chama cha Chadema, wilayani Shinyanga . Siri anaeleza kwamba, mwaka 2010 aligombea nafasi ya udiwani katika kata ya Chamaguha na hakufaulu, hivyo kujitosa kwenye viti maalumu na kufanikiwa kushinda kiti hicho.

Anasema, mwaka 2015 alihamia chama cha ACT-Wazalendo na aligombea nafasi ya uenyekiti Mkoa wa Shinyanga, haya alifanikiwa kuwashinda wanaume na hadi sasa, ni mwenyekiti wa chama hicho.

"Sifa ya mtu ili uwe kiongozi bora, lazima ujiamini, kusoma katiba ya chama chako, katiba ya nchi na kufanya utafiti kuyajua makubwa, ambaye ni kero za wananchi zinazohitaji kutatuliwa. Ukifanya hivyo, kamwe huwezi kushindwa kuongoza," anasema Yasini.

"Mimi nimefanikiwa kwenye uongozi wangu kutokana na kufuata misingi hiyo ya kusoma Katiba ya chama na Katiba ya nchi, pamoja na kujua matatizo ya wananchi na kuyatatua, na kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka huu (2020) lazima nichukue fomu ya kugombea ubunge katika jimbo la Shinyanga mjini,

> "Mwaka (2005 hadi 2010) nilikuwa diwani wa viti maalumu na baada ya kuonekana na kubadilika na wananchi, ikabidi mwaka 2010 nijitose kugombea nafasi ya udiwani kwenye kata ya Kolandoto.

"Kutokana na nafasi hii niliyonayo ya uenyekiti wa ACT-Wazalendo mkoa Shinyanga, huwa nafanya mikutano ndani ya chama kuwahamasisha wanawake wenzagu wajitokeze kwa wingi kugombea nafasi za uongozi na wasiogope, huku nikijitolea mfano mwenyewe namna ninavyojiamini na kuchapa kazi," anaongeza



Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, akizungumza.

### DC SHINYANGA

Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, anasema, siri ya mafaniko ya uongozi ni kushirikiana na wenzake, kujituma kazini, kutatua matatizo ya wananchi kwa kuwafuata huko walipo, kufanya mikutano ya hadhara, kuzingatia sheria za nchi na miongozo pamoja na kutii katiba ya nchi.

Mboneko anaeleza, amekuwa kiongozi tangu anasoma na baadaye, alikuwa kati ya mwaka 2016-na 2018, alikuwa Katibu Tawala wa Wilaya ya Dodoma, na akija aliteuliwa kuwa Mkuu wa Wilaya Shinyanga, akiongoza manispaa za Shinyanga na Shinyanga vijijini.

"Siri ya uongozi ni malezi kuanzia ndani ya familia. Ukiangalia sisi wanawake ndio huwa walezi wa familia zetu, hivyo tunapopata nafasi hizi za uongozi, huwa ni watendaji wazuri sana katika kuwatumikia wananchi kutatua kero zao, pamoja na kuwaletea maendeleo," anasema Mboneko.

"Siri nyingine ya mafanikio yangu ya uongozi ni kutokaa ofisini, bali huwa naenda 'field' (maeneo y tukio) kusikiliza kero za wananchi na kuzitatua, pamoja na kufuatilia utekelezaji miradi ya maendeleo kwa kuisimamia, ili ikamilike kwa wakati na kutoa huduma kwa wananchi, pamoja na kuwabana wabadhirifu wa fedha za miradi na kuzitapika," anaongeza.

### RC TELACK

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack, anasema Siri ya mafanikio yao katika utendaji kazi ni kuzingatia ushirikiano na walio chini yake, akitaja baadhi wakuu wa wilaya na Katibu Tawala wa Mkoa.

Anaeleza falsaga yake kwamba, mtu anapotakiwa kufanikiwa madarakani, ni sharti afanikiwe kwenye uongozi wake na kuwaheshimu wa chini yake na kufanya nao kazi.

"Siri ya mafanikio yangu mimi Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, ambaye ni kiongozi mwanamke ni kufanya kazi kwa ushirikiano na wenzangu, kushughulikia matatizo ndani ya jamii, pamoja na kuweka miundombinu ya kukuza uchumi wao kupitia uhamasishaji wa uwekezaji wa viwanda," anasema Telack.

"Mimi kama kiongozi mwanamke, kuna changamoto ambazo huwa nazipitia kwenye utendaji wangu kazi, ukizingatia nafasi yangu ni kusimamia shughuli za utekelezaji wa maendeleo na ninapowajibisha watu wazembe, lazima wanichukie na kunisema vibaya," anasema Telack anaendelea kujigamba: "Lakini, bahati nzuri wanawake hua tunamisimamo ndio maana nafanikiwa kwenye kazi zangu."


Pia anatoa msukumo kuwataka wanawake wajitokeze kugombea nafasi za uongozi kwenye uchaguzi mkuu mwaka huu, ili kuwepo uwiano sawa wa nafasi za uongozi kijinsia zote,

Anawataka wanawake kuwa wachapakazi wazuri na katika hilo anawahidi kuwaunga mkono wote watakaoathubutu kujitokeza kugombea uongozi.

"Katika kuelekea kwenye uchaguzi mkuu mwaka huu wa kuchagua madiwani, wabunge na Rais, natoa wito kwa wanawake mkoani Shinyanga wajitokeze kwa wingi kugombea nafasi za uongozi na mimi Mkuu wa Mkoa naahidi kuunga mkono mwanawake, ambaye atathubutu,"ameeleza Telack.

Msimamizi wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa katika Manispaa ya Shinyanga, Charles Kafutila, anataja matokeo ya uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka jana, kuwa wanawake hawakujitokeza kwa wingi kugombea nafasi za uongozi na wameishia kuambulia viti vichache kwenye uongozi.

# Bunge Marekani linavyokerwa na mipango ya Rais wao Trump



Kikao cha Bunge kikiendelea. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**Na Ani Jozeni**

VUTA nikuvute inaendelea nchini Marekani kuhusu mipango ya makao makuu ya Jeshi la Marekani, kupunguza au kuondoa sehemu kubwa ya vikosi vya Marekani vilivyoko barani Afrika, huku maofisa wa Pentagon (makao makuu ya jeshi) wakitazamia kuwa marafiki wa Marekani barani Ulaya wanaweza kusimamia eneo hilo.

Maofisa wa ngazi za juu waliohojiwa na vyombo vya habari hivi karibuni, walisema Waziri wa Ulinzi wa Marekani, Mark Esper, anadhani nchi za Ulaya zenye uhusiano wa jadi na Afrika, zinaweza kuchukua nafasi hiyo, ili Marekani ielekeze nguvu kwingineko.

Hapo hasa ni Mashariki ya Kati, na ikishindana na China, Russia. Inaelekea kuwa wabunge nchini humo, kwa mabaraza yote mawili, la Wawakilishi na Senate wana shaka kubwa na mpango huo wa Pentagon, hasa kutokana na ushindani ambao unaongeka kwa kasi katika eneo la Asia-Pacific.

Waziri Esper anaripotiwa kuwa ameangalia kila eneo la kimapigano, mikakati yake na majukumu halisi, na yuko mbioni kutoa maamuzi kama washirika wa Marekani wanaweza kuchukua nafasi kubwa zaidi katika mahitaji ya ulinzi na usalama wa maeneo hayo, hasa kuhusiana na ugaidi.

Eneo lililotajwa zaidi katika kuangalia upya nafasi ya Marekani kijeshi duniani ni Kamandi Maalum ya Afrika, inayochukua eneo lote la Afrika, isipokuwa Misri - ipo chini ya Kamandi Kuu ya Jeshi la Marekani, na manowari zake.

Hisia hiyo ni mwendelezo wa hatua ya Rais Donald Trump kuondoa vikosi vya Marekani katika mpaka wa Uturuki na Syria ambavyo kimsingi, vilikuwa vinawalinda wa-Kurdi dhidi ya Syria kwa upande mmoja na Uturuki kwa upande mwingine, kuacha kundi hatarishi la Dola ya Kiislamu nchini Irak na Syria.

Ni hatua illiyowashangaza wengi na kutoa nafasi kwa wataalamu Ulaya na Mashariki ya Kati kuanza kupambanua taswira mpya ya mahusiano ya kimataifa, kuwa nchi zenye ukaribu wa kijeshi, ulinzi na Marekani zianze kujitafakari.

> “Iran ilishambulia kwa makombora kambi mbili za kijeshi za Marekani nchini Irak na ‘kupandisha utambi’ wa uwezekano wa kutokea mfarakano mpana zaidi ya hapo.



Rais Donald Trump, alipokuwa bungeni mwaka 2018.

Hapo zifikirie zaidi kujitegemea, kwani Marekani haitabiriki na itatanguliza tu maslahi yake yenyewe huku ikiziacha nchi taabani.

Rais Trump ndiye aliyetoa maelekezo ya awali ya kufanya mapitio ya mikakati ya kijeshi ya Marekani katika maeneo kadhaa duniani, kwa msingi kuwa ni muhimu kuyaondoa majeshi ya Marekani katika vita vya kijinga visivyoisha, vingi vya kikabila na kuwarudisha askari wa Marekani nyumbani.

Licha ya wao kuwa maofisa wa juu wa Pentagon, wanasema hakuna uamuzi kamili uliofikiwa hadi sasa na, tayari kuna wimbi la kuhoji mwelekeo huo kutoka pande zote mbili za Bunge la Marekani.

**HOFU ILIYOKO**

Baadhi ya wabunge wanahofia kuwa Marekani itajiweka pembeni na kuziacha Russia na China, zijitanue zaidi kuamua nini kinatokea (au serikali gani zinaingia madarakani) na kunufaisha makundi ya kigaidi diniani kama Al Qaeda na Dola ya Kiislamu.

Seneta wa chama cha Republican, ambaye ni mjumbe wa Kamati ya Senate ya masuala ya kijeshi, alisema ni mtazamo finyu kupunguza kwa nguvu vikosi vya Marekani, kwa kuwa hali hiyo itapunguza uwezo wa Kamandi ya Afrika (Africom)l kutimiza majukumu yake.

Kwa vile seneta huyo ni mtu wa karibu na utawala wa Rais Trump, ilionekana alichosema kitatiliwa maanani na wapanga sera katika Pentagon na washauri wengine wa karibu wa Trump. Kuna seneta mwingine, naye pia wa karibu na Trump, aliyemwandikia barua Esper kuelezea hali hiyo.

Wakati Pentagon inaangalia uwezekano wa kupunguza kwa nguvu uwepo wa vikosi vya Marekani barani Afrika, mashambulizi ya kigaidi yamekuwa yakiongezeka kutoka Kenya hadi Niger na baadhi ya maeneo yanaanza kuwa na magaidi wa kudumu kama Kaskazini mwa Msumbiji.

Ugunduzi wa gesi na uwezekano wa kuwepo mafuta, kunasemekana kunachochea hali hiyo, kuzusha tamaa au matumaini kuwa vita ya ugaidi ikipiganwa kwa nguvu, itaishia kuunda serikali za shirikisho, ambako majimbo yanashika rasilimali za maeneo husika.

Pia, siyo serikali ya kitaifa na kwa maana hiyo wadau wa maeneo hayo watafaidika. Ni moja ya sababu za vita visivyoisha vya makundi ya wapiganaji nchini Jamhuri ya Kidemokrasi ya Msumbiji (DRC), inapotaka serikali isiwaingilie pindi wanapochimba madini.

Tayari mwaka huu Marekani, imeshapoteza askari wawili ambao ni waajiriwa wa kampuni zinazopewa tenda za ulinzi na usalama walioshambuliwa nchini Kenya. Wauaji ni kundi la kigaidi la Al Shabaab, lenye uwezo mkubwa wa kushambulia nje ya Somalia.

Hali hiyo bado haijagusa hisia za maofisa wa juu wa Pentagon ambao wanataka uwezo wa kijeshi wa Marekani uelekezwe zaidi katika eneo pana la Asia na Bahari ya Pacific, nje ya maeneo muhimu ya miaka mingi kwa mfano eneo lote la Mashariki ya Kati na sehemu kubwa ya Asia Kusini.

Bado si rahisi kuona nini hasa Pentagon inataka Mashariki ya Mbali, kwani ziko manowari za Marekani na kila mara vikosi vya Marekani vinafanya mazoezi ya pamoja na Japan au Korea ya Kusini, si vita.

Wakati uondoaji askari Marekani katika maeneo ya vita vya kikabila kwa, mfano kati ya makundi yenye madhehebu tofauti yanayopigania utawala nchi za Mashariki ya Kati, Waziri Esper emepeleka maelfu ya askari wa ziada, baada ya mvutano na Iran uliodumu miezi kadhaa hadi shambulio la ndege nyuki (droni).

Ni uharamia uliomuua kamanda wa vikosi maalum vya Quds , Meja Jenerali Qassem Soleimani, vyenye dhamana ya kuendesha mapigano katika nchi za Irak, Syria, Lebanon na Yemen.

Iran ilishambulia kwa makombora kambi mbili za kijeshi za Marekani nchini Irak na ‘kupandisha utambi’ wa uwezekano wa kutokea mfarakano mpana zaidi ya hapo.

**MAJESHI AFRIKA**

Kwa takwimu za hivi sasa, Pentagon inasemekana ina askari 6,000 barani Afrika, kiasi cha 1,400 kati yao wakiwa na makambi katika Afrika Magharibi, hasa nchini Niger, kwa mujibu wa kamanda mmoja mwenye cheo cha kanali katika Jeshi Kikosi cha Anga cha Marekani.

Kiasi cha askari 4,000 wako Afrika Mashariki na zaidi nchini Djibouti na kati ya askari 650 na 800 wako Somalia, ambako Marekani, kimsingi inatoa ushauri kwa vikosi vya nchi za Afrika vinavyopambana na Al Shabaab.

Moja ya njia ambazo Pentagon inatazamia kutumia huku ikipunguza uwepo wa makambi makubwa ya kijeshi, ni kuweka miundombinu zaidi ya kupeleka askari eneo maalum kwa haraka na kuondoka. Ni hali ambayo maofisa wanasema itaiwezesha Marekani kuingilia ki



## HABARI MBEYA

# Mbarali yaanza mkakati ujenzi wa madarasa

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

HALMASHAURI ya Wilaya ya Mbarali, imesema imeanza kujenga shule za sekondari mpya tisa katika mwaka huu wa fedha, ili kumaliza tatizo la uhaba wa vyumba vya madarasa ambayo imekuwa ikijitokeza kila mwaka.

Uamuzi huo ulitangazwa juzi na Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Francis Mtega, wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri hiyo kilichokuwa kimelenga kujadili makisio ya bajeti ya mwaka wa fedha 2020/2021.

Mtega alisema halmashauri hiyo imekuwa ikikabiliwa na tatizo hilo la upungufu wa vyumba vya madarasa kila mwaka baada ya matokeo ya darasa la saba kutangazwa na kwamba wengi huwa wanachelewa kuanza masomo kutokana na tatizo hilo.

Alisema mwaka 2019 halmashauri hiyo ilikumbwa na uhaba wa vyumba vya madarasa 37 hali ambayo iliwafanya watumie nguvu nyingi kukabiliana na tatizo hilo na mwaka huu bado tatizo ni kubwa kwa maelezo kuwa kuna upungufu wa vyumba 36.

Alisema wameamua kujenga shule hizo mpya ambazo ndizo zitakuwa suluhisho la kudumu la tatizo hilo na hivyo akawaomba wananchi wa wilaya hiyo kutoa ushirikiano kwa halmashauri wakati wa kutekeleza miradi hiyo.

"Ni kweli tunakabiliana na tatizo kubwa la uhaba wa vyumba vya madarasa lakini tumeona badala ya kuongeza vyumba hivyo ni bora tujenge shule mpya ambazo ndio itakuwa suluhisho la kudumu kwa tatizo hili," alisema Mtega.

Alisema tatizo la uhaba wa vyumba vya madarasa linasababishwa na hamasa kubwa ya wazazi kuwapeleka watoto wao shuleni baada ya kuanza kutekelezwa kwa Sera ya Elimu hila malipo nchini.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Kivuma Msangi, alisema kwa kuanzia mwaka huu wanatarajia kusajili shule mpya tano ikiwa ni utekelezaji wa maazimio ya Baraza la Madiwani.

Alisema katika wilaya hiyo kuna shule za msingi 115, lakini shule za sekondari zilizopo ni 18 pekee na kwamba ndio maana wameamua kujenga shule mpya ambazo ndizo wanapambana nazo katika kipindi hiki.

Baadhi ya madiwani wa halmashauri walisema tayari wamesharidhia uamuzi huo lakini tatizo litaanza kwenye utekelezaji na hivyo wakawaomba wananchi wa wilaya hiyo kushirikiana na serikali kwenye utekelezaji wa miradi hiyo.

Mmoja wa madiwani hao, Tupzketi Seperwa, aliwaomba wananchi hasa wa jamii za wafugaji kushiriki kwenye miradi hiyo hata kwa kuchangia chochote endapo watakosa nafasi ya kushiriki moja kwa moja.

Alisema shule hizo hazijengwi kwa ajili ya viongozi wa halmashauri bali ni kwa ajili ya watoto wao wenyewe na hivyo kila mmoja lazima ashiriki ili kufikia lengo.

# Shule maalum sasa kila halmashauri

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

SERIKALI mkoani Mbeya, inakusudia kujenga shule maalumu za sekondari katika kila halmashauri ambazo zitakuwa zinapokea wanafunzi waliofeli mitihani ya kidato cha nne kwa kupata madaraja ya sifuri na nne ili warudie kufanya mitihani.

Hayo yalisemwa juzi na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, wakati wa kikao cha wadau wa elimu mkoani humo kilichokuwa kimelenga kuwapongeza walimu na wanafunzi waliofanya vizuri kwenye mitihani mbalimbali ya taifa.

Chalamila aliwaagiza Maofisa Elimu Sekondari na Msingi wa Wilaya kwa kushirikiana na walimu kuandaa mpango wa ujenzi wa shule hizo ambazo zitakuwa za bweni na kuwasilisha ofisini kwake kabla ya Machi 15 mwaka huu ili utekelezaji wake uanze haraka.

Alisema wanafunzi watakaojiunga na shule hizo watakuwa wanasoma miaka miwili yaani kidato cha tatu na nne kisha wanafanya mtihani wa kidato cha nne na wakifanya vizuri waendelee na hatua zingine za masomo.

Alisema wanafunzi watakaojiunga na shule hizo watakuwa wanalipa ada ambayo itapendekezwa na kwamba mzazi yeyote ambaye mtoto wake atajiunga na shule hizo na akakataa kutoa ushirikiano atachukuliwa hatua za kisheria.

"Katika kipindi cha miaka mitatu, katika mkoa wetu wanafunzi waliopata division III (Daraja la tatu) wako 2,930 na waliopata division IV wapo 9,450 ambao hatujui wanapotelea wapi," alisema Chalamila na kuongeza:

"Sasa nimekuja na wazo, kwa kuwa tuna shule ambazo zinapokea wanafunzi waliofanya vizuri, sasa tuje pia na shule za wanaofanya vibaya yaani wanaopata division ziro na four mbaya katika kila halmashauri na nina uhakika hizi shule zitakuwa za mfano kwa Tanzania nzima."

Chalamila alisema kuna uwezekano mkubwa kuwa vibaka wengi ambao huwa wanawasumbua wananchi mitaani ndio hao waliomaliza kidato cha nne na kupata madaraja hayo duni kwenye mitihani yao ya taifa.



Mganga Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Dk. Mariamu Ngwere, akitoa taarifa za ujenzi wa zahanati ya kijiji cha Kyangala, wakati wa ziara ya Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Mbeya, jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wavamizi vyanzo maji wachongewa

**Na Innocent Ng'oko, MBEYA**

BAADHI ya wananchi wameiomba serikali kuharakisha utaratibu wa kuwaondoa watu wanaoharibu vyanzo vya maji katika wilaya ya Mbarali hususani katika eneo la Mnazi linalotumika kwa ajili ya shughuli za kilimo cha mpunga.

Hali hiyo inahatarisha jitihada za serikali katika ujenzi wa mradi mkubwa wa umeme wa maji wa Julius Nyerere katika bonde la Rufiji.

Walisema jana kuwa kiwango kikubwa cha maji kwa ajili ya mradi huo mkubwa wa maji wa Julius Nyerere ambao unatarajiwa kuzalisha megawati 2115 unategemea maji mengi kutoka vyanzo vingi vya mito inayounganisha Mto Ruaha katika Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya.

Nura Joseph, alisema kuwa ukitembelea eneo la mnazi kuna mashamba mkubwa ambayo yameanzishwa na wakulima mia ka ya hivi karibuni, ambapo wakulima wengi wamechimba mifereji mikubwa kutoka ndani ya mito inayotililisha maji ndani ya Mto Ruaha mkuu.

Alisema kuwa mbali na uchimbaji holela wa mifereji pamoja na kilimo kisichozingatia mpangilio kuna hatari kubwa ya shughuli hizo za kilimo zikaathiri jitihada za serikali za ujenzi wa mradi wa umme wa maji wa Julius Nyerere unaojengwa na serikali ya awamu ya tano kwa fedha nyingi katika eneo la Bonde la Rufiji.

Aidha, walisema kuwa kusuasua kwa mamlaka za serikali kuchukua hatua za haraka za kuwaondoa baadhi ya wakulima katika eneo hilo la Mnazi licha ya kuundwa kwa tume ya Makamu wa Rais na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kunatokana na baadhi ya vigogo wa serikali wanajihusisha na shughuli za kilimo katika eneo hilo.

Walisema eneo la Mnazi linatajwa kuwa na ukubwa wa hekari 16,000 zinazofaa kwa ajili ya shughuli za kilimo, ambapo miaka ya hivi karibuni baadhi ya wananchi wakiwamo vigogo ndani ya serikali walivamia eneo hilo na kujishughulisha na shughuli za kilimo cha mpunga.

Pia walisema eneo hilo limekuwa na mgogoro kati ya serikali na wakulima hao kutokana na uchimbaji holela wa mifereji ambapo kwa kiasi kikubwa imekuwa ikiathiri vyanzo vya umeme katika mabwawa ya Mtela na Kidatu kwa muda mrefu.

Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Rubeni Mfune na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, kwa kushirikiana na kamati za ulinzi na usalama wamekuwa wakiwazuia wakulima hao kuharibu vyanzo vya maji kutoka na uchimbaji holela wa mifereji na matumizi ya majenereta ambayo yamekuwa yakitumika kufyoza maji katika vyanzo hivyo vya mito.

Desemba mwaka 2018 Mkuu wa Mkoa wa Mbeya akiwa na kamati ya ulinzi na usalama alilazimika kufukia baadhi ya mifereji ambayo iliyoonekana kuathiri ikolojia ya Mto Ruaha Mkuu kutokana na kushuhudia uharibifu mkubwa uliofanywa na wakulima hao na kutishia jitihada za serikali za ujenzi wa mradi wa umeme wa maji wa Julius Nyerere katika eneo la Bonde la Rufiji.

Kwa mujibu wa taarifa ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, idadi ya wakulima wanaolima katika eneo hilo la Mnazi wanafikia 600, huku akibainisha kuwa idadi ya wakulima wanaomiliki eneo hilo ni wakulima wakubwa wanaofikia 50 ambao wamehodhi maeneo makubwa ya ardhi ambayo hayajawekewa miundombinu bora.

Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Ruben Mfune, alisema jana kuwa wanasubiri mapendekezo ya tume ya Rais ya mawaziri 8 waliofika katika wilaya hiyo, mwaka 2019, kwa lengo la kufuatilia athari za uharibifu huo wa vyanzo vya maji unaofanywa na wakulima.

Alisema serikali imefanya jitihada za kuwazuia watu wengine wasiendelee kumega maeneo ambayo yapo kwenye vyanzo.





# Asasi za kiraia zapewa onyo

**Na Peter Mkwavila, DODOMA**

VIONGOZI wa asasi za kiraia nchini wametakiwa kuhakikisha misaada inayotolewa na wafadhili inawafikia walengwa badala ya kujinufaisha wao binafsi.

Ofisa Maendeleo Jamii wa Jiji la Dodoma, Sharifa Nabalang'anya, amesema serikali haitazifumbia macho asasi za kiraia zitakazofanya shughuli zake bila kufuata sheria ikiwamo ya kusajiliwa.

Licha ya kibano kwa asasi hizo kufanya kazi bila usajili, wasimamizi wake watashtakiwa kwa mujibu wa sheria za nchi.

Pamoja na tahadhali hiyo, pia ameziagiza asasi hizo katika Jiji la Dodoma kuwakilisha taarifa zao za kila robo ya mwaka kwenye ofisa hiyo kwa lengo la kutaka kutambuliwa utendaji wao.

Hatua hiyo imekuja kutokana na maelezo kwamba ni muhimu asasi hizo zitambuliwe kazi zao zinazofanyika katika jamii kwa kitengo cha Ofisa Maendeleo ya Jamii.

Agizo hilo alilitoa alipokuwa akizungumza na wamiliki wa asasi na kusema kuwa pamoja na serikali kutambua umuhimu wa asasi za kiraia, lakini zinatakiwa kutambua kuwa ni muhimu kuwasilisha taarifa zao katika ofisi ya Halmashauri ya Jiji.

"Tunajua asasi za kiraia zinafanya kazi kubwa katika jamii ikiwamo pia serikali, lakini jamii haitambui kazi hizo kwa undani na wakati mwingine hata Halmashauri ya Jiji la Dodoma haizijui.

Pamoja na kuwapo kwa utaratibu wa asasi za kiraia kuwasilisha taarifa zao za utendaji kila baada ya robo mwaka, pia zimetakiwa kutumia vyema pesa ambazo zinatolewa na wafadhili badala ya kufanya ujanja ujanja.

Alisema asasi hizo zinatakiwa kuyafikia makundi mbalimbali kama vijana wanaojihusisha na dawa za kulevya, kuvuta bangi na vijana waishio vijiweni kujitambua na kuachana na tabia hizo badala yake wajishughulishe na kazi za kujiingizia kipato.

"Asasi za kiraia mnatakiwa kutambua kuwa nyie ni msaada mkubwa ndani ya serikali na mmekuwa msaada mkubwa kwa maana hiyo, naomba mtambue kuwa mnatakiwa kuyafikia makundi maalum," aliongeza.

**"Tunajua asasi za kiraia zinafanya kazi kubwa katika jamii ikiwamo pia serikali, lakini jamii haitambui kazi hizo kwa undani na wakati mwingine hata Halmashauri ya Jiji la Dodoma haizijui.**

# Wavuvi Mtera walalamika kuvunjiwa mitumbwi yao

**Na Peter Mkwavila, MPWAPWA**

WAVUVI wa bwawa la Mtera katika kambi ya Mwakibwera, wamelalamika kuvunjiwa mitumbwi 17 na watumishi wanaokusanya mapato wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa licha ya kuwa na leseni za kufanya uvuvi.

Malalamiko hayo waliyatoa jana walipokuwa wakizungumza na waandishi wa habari kwenye kambi hiyo.

Akizungumzia tukio hilo, mvuvi Joseph Mgeni alisema watumishi hao wameharibu mitumbwi 17 na kuwasababisha hasara ya Sh. milioni 5.1.

"Wametusababishia umaskini zaidi kutokana na kukosa kipato ambacho tulikuwa tunajipatia kwenye shughuli hizi za uvuvi, tunashangaa kuvunjiwa vitendea kazi vyetu wakati tumelipia leseni na tunafanya kazi kihalali," alisema.

Naye Hussein Mkwizu, alisema watumishi hao sita walivamia kambi hiyo wakiwa wamebeba mashoka na kuvunja mitumbwi.

"Hakuna mvuvi anayemiliki mtumbwi bila kulipia leseni kwa kuwa tusipolipa tutakuwa tunakiuka sheria na kanuni za biashara na kuibia mapato ya halmashauri," alisema.

Aliongeza: "Hatua waliyoichukuwa inaweza kusababisha maafa yasiyo na tija kitendo hichi hakivumiliki, Rais wetu anahimiza ufanyaji kazi kila mtanzania kwa ajili kujipatia kipato na kuinua uchumi sasa kwa hali hii iliyofanywa na watumishi hao wa serikali ni halali kweli?"

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Mtera, Simon Lukuwi, alisema hajashirikishwa juu ya uvunjaji wa mitumbwi ya wananchi wake.

Alisema kuwa watumishi hao wamekiuka sheria na hawakustahili kuchukua hatua hiyo bila kumshirikisha yeye na wavuvi hao.

Akizungumzia hilo, Diwani wa kata hiyo, Amon Kodi, alisema taarifa ya kuvunjiwa mitumbwi hiyo aliipata kutoka kwa wananchi kuwa kuna watumishi wa halmashauri ya Mpwapwa wanaokusanya mapato wamewavunjia mitumbwi kwa madai ya kutolipiwa leseni.

"Kisheria hawaruhusiwi kuvunja mitumbwi bali wanatakiwa kukamata chombo na kikikaa kwa siku 90 baada ya hapo anatakiwa kwenda mahakamani kuomba mahakama kwa ajili ya kuteketeza kwa kuchoma moto mitumbwi au nyavu," alisisitiza.

Nipashe ilimtafuta Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Daudi Sweha, ili kujua kuhusu tukio hilo ambapo alisema atalifanyia kazi kwa kuwa bado hana taarifa nalo.



Wavuvi wanaofanya shughuli zao katika Bwawa la Mtera, kambi ya Mwakibwera, mkoani Dodoma, wakiangalia mitumbwi yao, juzi, inayodaiwa kuvunjwa na watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa kutokana na kutolipia leseni. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Wilaya 20 zinakabiliwa na udumavu kwa watoto

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

IMEELEZWA kuwa zaidi ya wilaya 20 nchini zinakabiliwa na tatizo la udumavu kwa watoto na wajawazito kutopata lishe inayostahili.

Uchunguzi uliofanywa na taasisi hiyo umeonyesha kuwa wilaya zaidi ya 20 zinakabiliwa na tatizo la udumavu kwa watoto na kinamama wajawazito kutopata lishe inayostahili.

Akizungumza na Nipashe jijini hapa Mjumbe wa Taasisi inayojihusisha na utoaji wa elimu kwa wanawake, vijana na watoto kuhusu masuala ya lishe na fistula (FUREO), Kelvin Haule, alisema kuwa wilaya hizo hali ya lishe ni asilimia 24 pekee, huku Wilaya ya Ruangwa ikiwa na asilimia 7 ya udumavu.

Alitaja wilaya hizo kuwa ni Mbarali, Rungwe, Kibiti, Rufiji, Bagamoyo, Halmashauri ya Chalinze, Ilala, Ubungo, Kilolo, Mufindi, Ruangwa, Nachingwea, Tandahimba, Wanging'ombe, Njombe, Ifakara, Kilolo, Magu, Chato, Geita, Halmashauri ya Shinyanga Manispaa na Kahama.

Alisema katika uchunguzi wao walibaini kuwa watoto wenye umri wa kati ya miezi sita hadi 23 wanakabiliwa na tatizo la lishe bora kutokana na kukosenaka kwa elimu ya kutosha matumizi ya bora ya vyakula.


"Hali ya lishe katika wilaya hizi hairidhishi kwani zipo kwenye asilimia 24 tu, na kati ya hizo wilaya yenye tatizo hili kwa kiwango kikubwa ni wilaya ya Ruangwa yenye asilimia 7 ikifutiwa na Tandahimba asilimia 6.8," alisema Haule.

Hata hivyo, alisema kutokana na hali hiyo wameamua kuanzisha mradi ambao watatekeleza kwa muda wa miezi nane katika wilaya hizo.

Alisema kila wilaya watafikia wananchi 120 na mradi unalenga kuongeza kiwango cha upatikanaji wa lishe kutoka asilimia 24 hadi kufikia asilimia 50 na utagharimu zaidi ya Sh. milioni 258.8.

Mkurugenzi wa taasisi hiyo, Davidi Msuya, alisema kupitia mradi huo watakomesha tatizo la fistula kwa wanawake na utapiamlo kwa watoto.

"Mradi huu umeanza leo na utahusisha wataalamu mbalimbali wa masuala ya afya," alisema.



# Viongozi wa dini waombwa kuelimisha jamii kuhusu usafi

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WAZIRI wa Afya Zanzibar, Hamad Rashid Muhammed, amewataka viongozi wa dini kuwahamasisha wananchi kuhusu suala la usafi ili kuepukana na maradhi mbalimbali.

Akizungumza katika mkutano wa viongozi wa dini ulioandaliwa na taasisi ya dini katika masuala ya afya na haki za watoto, (Tanzania Interfaith Partnership TIP) uliofanyika Mazizini nje ya Mji wa Zanzibar, alisema kuwa dini zote zinasisitiza suala la usafi, hivyo ni vyema viongozi hao kutoa elimu kwa waumini wao kuhusu suala hilo.

Alisema msingi mkubwa wa matatizo ni kutokutembea na maandiko ya dini na ndio maana baadhi ya viongozi wa dini wamekuwa wakivunja sheria na kujiingiza katika vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia.

Alisema serikali inajitahidi kuweka misingi ikiwamo kuwa na katiba na sheria za nchi, lakini baadhi yao wamekuwa hawaziheshimu sheria hizo.

"Tumepitisha kanuni nzuri za matumizi ya maji, lakini je, tunazifuata? Unatoka nyumbani huoshi hata mikono," alisema.

Alisema umefika wakati sasa jamii kubadilisha mitazamo yao na kulipa umuhimu suala la usafi ili kuepukana na maradhi mbalimbali ikiwamo ya mlipuko.

Aliwataka viongozi hao kutoa elimu ya usafi kwa watoto ambao ndio watakaoleta mabadiliko na elimu hiyo ianze kutolewa shuleni.

Waziri huyo alisema viongozi wa dini wana nafasi kubwa ya kutoa elimu kwa jamii, lakini baadhi yao wamekuwa wakijiingiza katika vitendo visivyokubalika katika jamii.

Alisema ushiriki wa serikali katika kutengeneza miundombinu mizuri ikiwamo upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama utasaidia kuimarisha suala la usafi.

Kwa upande wao viongozi wa dini walisema wao ni vioo katika jamii na wana ushawishi mkubwa hivyo watalifanyia kazi suala la utoaji wa elimu kuhusu usafi ili kuimarisha mazingira.

Fadher Filipo Munguti, mratibu wa vijana wa elimu ya Kikristo, alisema kuwa mabadiliko hayaji mara moja hivyo nguvu kubwa ya utoaji elimu ya usafi wataelekeza kwa watoto.

Abdallah Hamid Suleim, mkufunzi wa Chuo cha Kiislamu Zanzibar, alisema kuwa afya ya jamii imemlazimu kila mwananchi na afya haitegemei dini wala siasa hivyo ni muhimu sana na inapokosekana afya amani inakosekana.

Naye Mkurugenzi wa taasisi nne za dini wa TIP, Halima Msomi, alisema kuwa viongozi wa dini wanasikilizwa sana katika jamii hivyo wameamua kushirikisha ili kuendana na mazingira.

Alieleza kuwa usafi binafsi na mazingira ni muhimu hasa suala la kuosha mikono baada ya kutoka chooni na kabla ya kula ili kuepukana na maradhi ya kipindupindu.

"Pia taasisi yetu imekuwa ikishughulika na usafi wa mtoto wa kike wakati anapokuwa katika hedhi ili kusaidiwa na kuweza kuhudhuria masomo shuleni na uhifadhi wa mazingira katika kuhifadhi taka na matumizi ya choo," alisema.



Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Mihayo Juma Nhunga (wa tatu kushoto), akimkabidhi baskeli mmoja wa watu wenye ulemavu, Haji Makame Khamis, wakati wa hafla ya makabidhino ya vifaa visaidizi kwa watu wenye ulemavu, Michezani mjini Zanzibar juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wafanyabiashara wapewa angalizo maradhi ya corona

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

KUFUATIA kuibuka kwa ugonjwa wa homa ya mafua makali unaosababishwa na kirusi kipya aina ya corona nchini China, wafanyabiashara wa Zanzibar wanaokwenda mchini humo, wameshauriwa kusitisha safari zao kwa kipindi hiki ili kunusuru afya zao.

Hayo yalielezwa na Waziri wa Afya, Hamad Rashid Mohamed, wakati akizungumza na Nipashe nje ya mkutano wa viongozi wa dini uliofanyika mjini Zanzibar.

Alisema kuwa Serikali ya Zanzibar kwa kushirikiana na Serikali ya Tanzania inafanya juhudi za pamoja kuweka kinga katika viwanja vya ndege ili kudhibiti virusi hivyo.

Alisema kuwa suala la kudhibiti wasafiri ni jambo la msingi sana kwa sababu Wazanzibari wanapenda kufanya biashara nchini China hivyo ni vizuri kuangalia kuwa wako salama.

Alisema China ni sehemu moja wapo nzuri ya kufanya biashara hivyo ni vyema wafanyabiashara wa Zanzibar kutoenda kwa kipindi hiki.

"Tahadhari ni jambo la msingi kwa eneo ambalo limeathirika... ni vizuri watu wakajizuia kipindi hiki mpaka serikali itakapotangaza kuwa China ni salama, hivi sasa wapumzike afya zao ni muhimu sana tunazihitaji," alisema Hamad.

Aidha, alisema wafanyabiashara hao wanaporudi na matatizo wanaweza kuwaambukiza watu wengine, na kuisababishia nchi kutokuwa salama.

Alisema wanaweza kwenda nchi zingine ambazo ziko salama kuendelea kufanya biashara zao hadi pale maradhi hayo yatakapoondoka.

**"Tahadhari ni jambo la msingi kwa eneo ambalo limeathirika... ni vizuri watu wakajizuia kipindi hiki mpaka serikali itakapotangaza kuwa China ni salama, hivi sasa wapumzike afya zao ni muhimu sana tunazihitaji," alisema Hamad.**

# Mawakala vyama siasa watoa neno uandikishaji

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MAWAKALA wa vyama vya siasa waliomo katika vituo vya uandikishaji wa daftari la kudumu na uhakiki kwa wapigakura, wameipongeza Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) kwa kuendesha zoezi hilo vizuri.

Wakizungumza na waandishi wa habari baada ya kutembelea vituo mbalimbali vilivyoko Wilaya ya Wete na Chakechake Kisiwani Pemba, walisema ZEC imejipanga vizuri na wananchi wanaokwenda vituoni humo kila mwenye sifa hupatiwa haki hiyo bila ya matatizo.

Khamis Othman Khamis wakala kutoka Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) na Faki Ali Mkadam wa Chama cha Wananchi (CUF), walieleza mwenendo huo wa tume, umewafanya mawakala kuwa na ushirikiano mkubwa baina yao na watendaji wa tume, hali ambayo inawafanya wananchi wanaokwenda kujiandikisha au kuhakikiwa taarifa zao kuchukuwa muda mfupi wa kumaliza taratibu zote za kuingizwa kwenye daftari. Walisema tume ya iendelee kutoa vitambulisho kwa wananchi ambao hawajapata hadi sasa ili nao waweze kupata haki yao ya msingi, ambayo itawafanya waweze kuchaguwa viongozi wanaowapenda.

Kwa upande wao wakuu wa vituo vya uandikishaji na uhakiki wa taarifa za wapigakura katika vituo vya Jimbo la Mgogoni, Jamali Kassim Shegwando na Hasnuu Faki Hassan, walisema hali ya uandikishaji inakwenda vizuri na watu wengi wanendelea kujitokeza vituoni.

Walieleza kuwa hadi sasa hakuna mwananchi yoyote ambaye amekwenda vituoni kutaka kujiandikisha ama kuhakiki taarifa zao kwenye daftari hilo akakosa kupatiwa haki hiyo.

Zoezi la uandikishaji wapigakura wapya na uhakiki wa taarifa za wapigakura waliomo katika daftari la kudumu linaendelea katika vituo 38 vya Wilaya ya Wete na majimbo matatu ya Wilaya ya Chakechake Pemba ambapo zoezi hilo linatarajiwa kuanza Februari 13, mwaka huu kisiwani Unguja.

# Diwani kizimbani tuhuma kutishia kuua

**Na Jumbe Ismailly, IGUNGA**

DIWANI wa Kata ya Kining'inila (CCM) Halmashauri ya Wilaya ya Igunga mkoani Tabora, Elisha Anthony, amependishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi wa Wilaya ya Igunga akikabiliwa na mashtaka mawili, likiwamo la kumtishia kifo Ofisa Mtendaji wa Kata ya Kining'inila, Fanty Mnyasa Haroun.

Ilidaiwa na Mwendesha Mashtaka wa Jeshi la Polisi Wilaya ya Igunga, Elimajidi Kweyamba, kwamba Anthony anakabiliwa na mashtaka mawili likiwamo la kutishia kuua kwa maneno kinyume cha kifungu cha 89 (2) (a) kanuni ya adhabu sura ya 16 mapitio ya 2002 inayozuia kutenda makosa kama hayo.

Mbele ya Hakimu wa Wilaya ya Igunga, Eddah Kahindi Kweyamba, alidai Januari 17, mwaka huu majira ya alasiri kwenye kata hiyo, kwa nia ovu mshtakiwa alimtishia Haroun kwa njia ya maneno kwamba atamuua.

Kwa mujibu wa Mwendesha Mashtaka huyo, katika shtaka la pili la mshtakiwa huyo ni kutumia lugha ya matusi kinyume cha kifungu 89(1) (a) kanuni ya adhabu sura 16 mapitio ya 2002.

Kweyamba alidai pia kuwa katika tarehe hiyo muda huo huo na maeneo hayo hayo, mshtakiwa alimtolea lugha ya matusi mlalamikaji kwa kumtolea maneno nakali ambayo ni kinyume cha maadili.

Hata hivyo, mshtakiwa alikana makosa hayo, hivyo kupelekwa mahabusu kutokana na kushindwa kutimiza masharti ya dhamana.

Kwa mujibu wa hati ya mashtaka hayo, mshtakiwa huyo alitakiwa kuwa na mdhamini mmoja ambaye ni mtumishi wa serikali na awe mkazi wa Igunga. Pia awe na barua ya mwajiri wake na kitambulisho cha Taifa na cha mpigakura pamoja na kuweka dhamana ya fedha taslimu shilingi milioni tano.

Kesi hiyo imeahirishwa hadi Februari 7, 2020 mwaka huu, itakapoanza kusikilizwa. Kutokana na mwendesha mashtaka kuieleza mahakama kuwa upelelezi wa shauri hilo umekamilika.



Wanafunzi wa kidato cha kwanza wa sekondari mpya ya Dan Mapigano Memorial ya Kata ya Bugoji, Musoma Vijijini, mkoani Mara, wakiingia darasani juzi, baada ya shule kuanza kupokea wanafunzi kuanzia Januari 16, mwaka huu. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

## Kampuni ya kuku yampa tano Kairuki

**Na Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI Mtendaji wa kampuni ya kitanzania ya AKM Glitters Limited ambayo inazalisha vifaranga na chakula cha kuku, Elizabeth Swai, amepongeza hatua ya serikali kutembelea viwanda vikiwamo vya kuzalisha kuku na kuwa hatua hiyo itasaidia kuleta ufumbuzi wa haraka wa changamoto zinazokwamisha sekta ya viwanda nchini.

"Kitendo cha Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Uwekezaji, Angellah Kairuki, kutembelea viwanda na kusikiliza changamoto mbalimbali tunazokabiliana nazo sisi wenye viwanda ni hatua njema kufikia uchumi wa kati na viwanda ifikapo 2025," alisema Swai.

Alisema kampuni yake ambayo ina uwezo wa kutotolesha vifaranga 106,000 kwa wiki na kuzalisha tani 200 za chakula cha kuku kwa siku, imekuwa ikikabiliana na changamoto mbalimbali za kimwingiliano kutoka mamlaka za udhibiti.

"Tunamshukuru sana Waziri Kairuki alipotembelea kiwanda chetu wiki iliyopita tulimweleza jinsi tunavyozalisha vifaranga, chakula cha kuku na pia changamoto mbalimbali tunakabiliana nazo katika majukumu yetu," alisema.

Katika ziara yake aliongozana na maofisa kutoka Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) ili wajionee na kufanyia kazi changamoto ambazo zipo ndani ya uwezo wao bila hata waziri kuingilia kati.

Swai alisema wamemwambia waziri kuwa kati ya mwaka 2017 na 2019 walikuwa wakitozwa kodi kila walipokuwa wakiingiza mbegu za kuku kutoka nje kitu ambacho kilikuwa kinyume cha sera.

"Tulimweleza waziri kuhusu barua mbalimbali zenye vitisho na mkanganyiko kutoka kwenye mamlaka za udhibiti," alisema na kuongeza kuwa waziri ameahidi kuzifanyia kazi changamoto zote ili kukuza na kuimarisha sekta ya viwanda.

Alisema yeye na menejimenti nzima ya kampuni wana imani kubwa sana na serikali katika azma yake ya kujenga uchumi wa kati na viwanda kama alivyokusudia.

Alisema Waziri Kairuki alifurahia sana jinsi kampuni inavyozalisha vifaranga vya kuku na kuwanufaisha wafugaji na wajasiriamali wengi vijijini ambako kampuni ina mawakala zaidi ya 400.

Kampuni hiyo ambayo ina kibali pekee cha kuingiza mama kuku (kuroirela) kutoka India ina wafanyakazi 78 na pia kinapokea wanafunzi wanaojifunza kwa vitendo zaidi 30 kwa wakati mmoja.

"Tunatotoresha au kuzalisha vifaranga eneo la Mbezi, shamba la mama kuku (kuroirela) Madale. Pia tuna mashamba ya chakula cha kuku Mbezi, Bagamoyo na Mkuranga," alisema Swai ambaye ni mwanzilishi wa kampuni hiyo.

# Wanavijiji 7,500 wapata ukombozi afya

**Na Jumbe Ismailly SINGIDA**

ZAIDI ya wakazi 7,500 wa vijiji vya Maghojoa, Mwakichenje, Ghata na Mipilo wanatarajia kuondokana na adha ya kutembea umbali mrefu kufuata huduma za afya Kituo cha Afya cha Kata ya Msange, baada ya ujenzi wa zahanati katika kata ya Maghojoa na Kata ya Mtinko kuanza.

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Singida, Dk. Lucas Juma Kazingo, aliyasema hayo kwenye hafla ya kupokea msaada wa vifaa vya ujenzi wa zahanati za kijiji cha Mwachambia katika Kata ya Maghojoa na Mwakichenje katika kata ya Mtinko vyenye thamani ya shilingi milioni tano zilizotolewa na Benki ya NMB.

"Zahanati ambazo bado zinajengwa na zinapatiwa mabati na mbao na Benki ya NMB ni zahanati ya Mwachambia iliyopo Kijiji cha Mwachambia Kata ya Maghojoa na Zahanati ya Mwakichenje ambayo ipo kata ya Mtinko, zahanati hizi bado zinajengwa, lakini pale wana shida ya huduma ya afya," alisisitiza Dk. Kazingo.

Kwa mujibu wa daktari huyo, wakazi wa Kijiji cha Mwakichenje na Kijiji cha Mwachambia wanapata huduma za afya kutoka katika Kituo cha Afya cha Kata ya Msange ambapo kuna umbali za zaidi ya kilomita 16 kwenda na kurudi, hivyo ili kuwanusuru na umbali huo mrefu, serikali imeamua kujenga zahanati katika vijiji hivyo.

Mwanahamisi Abdalah Irunde, mkazi wa Kijiji cha Mwakichenje alizitaja changamoto zingine ni kunyanyaswa na wahudumu wa afya wanaotoa huduma hizo katika Kituo cha Afya Kata ya Msange sambamba na kupatiwa huduma duni katika kituo hicho kilichoko jirani na kijiji chao.

Naye mkazi wa Kijiji cha Mwakichenje, Pendo Julius, alisema kwamba wanawake wa kijiji hicho hutembea umbali mrefu kufuata huduma za kliniki, huku kukiwa na wanawake wanaokwenda kufuata huduma za kujifungua ambao hujikuta wakijifungulia njiani.

Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Kati, Nssolo Mlozi alibainisha maeneo manne ya benki hiyo ya kujitolea kurudisha kwa jamii kuwa ni sekta ya elimu, afya, kutoa elimu ya masuala ya fedha na majanga.

Alisema katika kipindi cha mwaka 2019 benki hiyo ilitenga jumla ya Sh. bilioni moja kwenye kitengo cha majanga.

Akipokea msaada huo, Mkuu wa Wilaya ya Singida, Pascas Muragiri, alivitaja vifaa hivyo ni mabati, misumari, nondo, makoa na mbao na kuongea kuwa Shule ya Msingi Msange ina upungufu wa vyumba vya madarasa 16 na matundu ya vyoo 34.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### MATANGAZO MCHANGANYIKO

**MKOPO WA HARAKA KUTOKA ENTERPRISE FINANCE LIMITD (EFL).** Kwa mahitaji kama kulipa ada ya shule, kodi, kuboresha biashara, kumalizia tenda etc. Kwa maelezo zaidi **piga 0758 112 332. Karibu EFL**.

**TANZANIA RESEARCH AND CAREER DEVELOPMENT INSITUTE:** Inatangaza mhula mpya wa masomo Certificate na Diploma za kilimo na maendeleo ya jamii.maelezo zaidi tembelea tovuti yetu www.tracdi.ac.tz Simu**:0714404491/0746995144**


***NIPASHE NI JIBU LAKO***

**NJOO UTANGAZE NASI**

**BIDHAA YAKO**

**KWA BEI NAFUU SANA**


### PASSPORT IMEPOTEA



NANCY AURELIA MAGERE anatangaza kupotelewa na Hati ya Kusafiria (Passport) yenye namba AB 283191. iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Makao Makuu Dar es salaam mwaka 2008.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu.

Taarifa ya polisi:
BUG/RB/7443/2018.

### HATI YA KIAPO
**KUKIRI KUPOTELEWA NA OFFER YENYE USAJILI WA PLOT NO.644 KITALU "B" NGAMIANI YENYE JINA LA bibi HILDA MSONDE:**

Mimi **LIGHTNESS FANUEL KIAZE** wa S.L.P TANGA, Mkristo mtu mzima na mwenye akili zangu timamu ninathibitisha kama ifuatayo.

1. Kwamba mimi ndiye muapaji nilietajwa hapo juu. Mmiliki halali kwa sasa wa kiwanja Na.644 Kitalu"B" Kilichopo katika eneo la New Nguvumali, kata ya nguvumali, Tanga Mjini.
2. Kwamba **OFFER, HIYO NINATHIBITISHA KUWA IMEPOTEA MIKONONI MWANGU MIMI LIGHTNESS FANUEL KIAZE.**
3. Kwamba nimejaribu kuitafuta kwa juhudi zangu sijafanikiwa nimetoa taarifa Polisi nakupatiwa **LOSS REPORT TAN/RB/85039/2020.**
4. Kwamba naiomba Ofisi ya Mipango Miji, pamoja na polisi Mkoa wa Tanga itambue upotevu huu na ninathibitisha imepotea mikononi mwangu mimi muapaji, nipo tayari kulipa kodi zote husika za serikali.
5. Kwa kiapo hiki naiomba Ofisi ya Mipango Miji inipatie hati ya kumiliki nyingine kwa jina hilo la marehemu **MZEE KHAMISS MWINDADI**

UTHIBITISHO; Nathibitisha kwamba maelezo niliyoyaeleza hapo juu ni ya kweli kweli tupu kadri nijuavyo kwa sheria za viapo.

LIGHTNESS FANUEL KIAZE

215603802

### ROYAL RUNNER'S AND GENERAL SUPPLIES T.LTD & COURT BROKER

**MNADA WA HADHARA**

UTAFANYIKA TAREHE 30/01/2020 SAA 4 ASUBUHI KWA IDHINI YA MAHAKAMA YA MWANZO MAKOLE WILAYA YA DODOMA MJINI TUTAUZA NYUMBA ILIYOKO ILAZO WEST PLOT NO.63 BLOCK F KWA AJILI YA MGAWANYO WA MALI.

**KWA MAWASILIANO PIGA**
**0713 - 913150**

IN THE HIGH COURT OF BUKOBA
AT BUKOBA
TAXATION CAUSE NO. 21/2019
TWAHA OMARY............DECREE HOLDER
VERSUS
LUKUMANI OMARY.........JUDGMENT DEBTOR

TO: LUKUMANI OMARY, KAGERA

**RE: NOTICE OF DATE OF MENTION**

Whereas the above mentioned decree holder lodged a case registered as Taxation cause No. 21 of 2019 against you at the high Court of Bukoba at Bukoba.

Take notice that the above said case has been scheduled for mention on 13th day of Feb, 2020 at 09:00 am before Hon. J.M. Minde. You are authorized to appear in person or through your Advocate.

Take further notice that in default of your appearance on that date and time for the said mention the case will proceed in your absence.

Given under my hand and seal of the Court this 27th day of JAN, 2020.

DEPUTY REGISTRAR
HIGH COURT OF TANZANIA
BUKOBA

215603302


*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Tupigie 0782253676*

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi***

***Kwa Bei Poa***

***Tupigie 0782253676***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# MAN UNITED KUMRUDISHA SANCHEZ KUTOKA INTER




**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United ipo tayari kumpa ofa Alexis Sanchez kurudi klabuni hapo na "kufufuka upya" kwenye dimba la Old Trafford wakati wa kipindi cha majira ya joto kijacho, kwa mujibu wa ESPN.

Sanchez anacheza kwa mkopo pale Inter Milan, lakini klabu hiyo ya Italia haina mpango wa kumnunua na mchezaji huyo wa kimataifa wa Chile anatarajiwa kurudi Julai mwaka huu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 amekuwa kwenye wakati mgumu klabuni hapo baada ya kutua akitokea Arsenal Januari 2018 na wakati United ikiwa imeacha milango wazi ya ofa kwa mchezaji huyo, wataendelea kuwa naye.

Mkataba wake wa mshahara wa pauni 500,000 kwa wiki unamalizika mwaka 2022 na Ole Gunnar Solskjaer ameambiwa anaweza kumjumuisha mchezaji huyo wa zamani wa Barcelona kwenye mipango yake msimu ujao.

Sanchez amekuwa akisumbuliwa na majeraha ya mara kwa mara tangu awasili kwa muda hapo kwenye dimba la San Siro na amefunga bao moja tu katika mechi sita alizoichezea klabu hiyo.

# Liverpool mdomoni mwa Chelsea FA Cup

**LONDON,** England

LIVERPOOL inaweza kukutana na Chelsea kwenye raundi ya tano ya Kombe la FA kama watashinda mchezo wake wa marudiano na Shrewsbury Town.

Kikosi hicho cha kocha Jurgen Klopp ambao ni vinara wa Ligi Kuu ya England walilazimishwa sare ya 2-2 na klabu hiyo ya daraja la tatu Jumapili.

'Wekundu' hao wanapewa nafasi ya kufuzu kwenye mchezo huo wa marudiano utakaopigwa pale Anfield, lakini watakabiliwa na wakati mgumu kwenye hatua ya 16 bora kwani wanaweza kukutana na vijana wa Frank Lampard wa pale Stamford Bridge.

Bingwa mtetezi wa taji hilo, Manchester City leo Jumatano watacheza na Sheffield Wednesday.

Arsenal itasafiri kwenda Portsmouth baada ya 'Washika Bunduki' hao kuwafunga Bournemouth kwenye mchezo uliopigwa Jumatatu.

Mechi zote nane zitachezwa katikati ya wiki ya Machi 3-5, mwaka huu.

**Ratiba kamili:**

Sheffield Wednesday v Manchester City
Reading/Cardiff City v Sheffield United
Chelsea v Shrewsbury Town/Liverpool
West Brom v Newcastle United/Oxford United
Leicester City v Coventry City/Birmingham City
Northampton Town/Derby County v Manchester United
Southampton/Tottenham v Norwich City
Portsmouth v Arsenal





# Newcastle yafikia pazuri sokoni

**NEWCASTLE,** England

MAZUNGUMZO juu ya uwezekano wa kuinunua Newcastle United kwa pauni milioni 340 na kampuni kutoka nchini Saudi Arabia yanaendelea "vizuri".

Makubaliano kati ya Kampuni ya Saudi ya Public Investment Fund (PIF) na mmiliki wa Newcastle, Mike Ashley yamekuwa na maendeleo mazuri kwa kipindi cha miezi michache iliyopita.

Nafasi ya makubaliano sasa yapo "kwenye nafasi nzuri zaidi" kwa mujibu wa mwanafamilia mmoja wa mmiliki wa klabu hiyo.

Lakini walionya kwamba mazungumzo yenyewe "ni magumu" na mpango huo bado unaweza kukwama.

"Ashley ahitaji kuuza, na hatabiriki," kilisema chanzo kimoja kutoka ndani ya familia hiyo.

Mwanamama mfanyabiashara na mtaalamu wa fedha, Amanda Staveley anaelewa wamezungumza na Prince Mohammed bin Salman wa Saudi Arabia kuhusu mpango wa kuinunua klabu ya Ligi Kuu ya England.

Staveley alishindwa kuinunua klabu hiyo miaka miwili iliyopita baada ya Ashley kusema alitaka kumalizika kipindi chake cha miaka 10 ya kuimiliki klabu hiyo.

# Kocha amwona Fernandes Man United

**LISBON,** Ureno

KOCHA wa Sporting CP, Silas hawezi kuthibitisha kama Bruno Fernandes anayetakiwa Manchester United amecheza mchezo wake wa mwisho kwa klabu hiyo ya Ureno juzi Jumatatu.

Licha ya kuhuishwa na United wakati huu wa dirisha dogo la usajili na katika madirisha yaliyopita, Fernandes amebakia Lisbon huku majaliwa yake yakiwa hayajulikani na alikuwa nahodha wa Sporting wakati wakiibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Maritimo.

Huku United na Sporting bado zikiripotiwa kujaribu kukubaliana kukamilika kwa dili hili kabla ya kufungwa kwa dirisha dogo la usajili, Silas kwa mara nyingine tena aliulizwa kuhusu majaliwa ya nahodha Fernandes.

"Siwezi kuthibitisha (kama Fernandes amecheza mechi yake ya mwisho dhidi ya Maritimo), ningependa yeye abakie hapa," alisema Silas akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo.

"Kwa sasa sijui kama atabakia au la, lakini ningependa kumhesabia kwenye timu yetu angalau hadi mwishoni mwa msimu huu.

"Bruno Fernandes ni mchezaji tofauti, anaona vitu ambavyo mtu mwingine hawezi kuviona.

"Timu yoyote ambayo ingekuwa na Bruno Fernandes nchini Ureno itakuwa na wakati mgumu ikimpoteza yeye. Kama ni hivyo, tutajaribu kuangalia suluhisho."

Kiungo huyo mwenye umri wa miaka 25, alifunga mabao 31 msimu uliopita, yakiwamo 20 kwenye Ligi Kuu ya Hispania, Primeira Liga.





# ARTETA AFUNGUKA USAJILI VIJANA ARSENAL 'WAKIUA'

**LONDON,** England

MIKEL Arteta alijisikia fahari kubwa wakati wachezaji wake vijana wa Arsenal wakifuzu raundi ya tano ya Kombe la FA baada ya kushinda dhidi ya Bournemouth.

Arsenal ambao ni washindi mara 13 wa taji hilo, walipata ushindi wa 2-1 kwenye dimba la Vitality kwa mabao ya Bukayo Saka na Eddie Nketiah kabla ya Sam Surridge aliyetokea benchi kufunga la kufutia machozi.

Mabao hayo mawili ya Arsenal yalipatikana wakati kikosi hicho cha vijana tupu kikionyesha kiwango cha kuvutia na safu ya ulinzi ya Arteta ilipata pigo baada ya kuumia kwa Shkodran Mustafi.

Arteta, hakiwa amefurahishwa na kiwango hicho cha Jumatatu, alibainisha kwamba, klabu yake itahitaji kuingia sokoni kwa ajili ya kuimarisha kikosi chake, na sasa watakutana na Portsmouth kwenye raundi inayofuata.

"Nimefurahishwa sana. Ilikuwa ni vigumu kuja hapa na kushinda, tumefanya hivyo na timu ya vijana," alisema bosi huyo wa 'Washika Bunduki' akiiambia BBC Sport.

# *Rodrigo anukia kumrithi Suarez*

**BARCELONA,** Hispania

RAIS wa Barcelona, Josep Maria Bartomeu amethibitisha kwamba mabingwa hao wa LaLiga wanafikiria kumsajili mshambuliaji wa Valencia, Rodrigo Moreno.

Rodrigo amekuwa katika rada za Barca, ambao wapo sokoni kutafuta mchezaji wa kuimarisha safu ya ushambuliaji baada ya Luis Suarez ambaye ni majeruhi kuelekea mwisho wake wa uchezaji.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania, Rodrigo, ambaye amefunga mabao 15 kwenye mashindano yote msimu uliopita, ameifungia mabao manne Valencia msimu huu. Alipoulizwa kuhusu uvumi huo, Bartomeu alisema: "Hatuwazungumzii wachezaji kutoka timu nyingine. Lakini (Rodrigo) jina lake lipo mezani kwa makocha.

Nahodha wa Barca na mshindi mara sita wa Ballon d'Or, Lionel Messi pia alikuwa sehemu ya majadiliano hayo.

Mwaka jana, Messi alisaini mkataba mpya na Barca ambao utamuweka hapo hadi mwaka 2021 na miamba hao wa Hispania pia wanataka kumwongezea mkataba mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32.

"Atakamilisha na Barcelona wakati atakapotaka. Mahusiano yake na Barcelona ni ya milele," alisema Bartomeu.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# ERIKSEN HATIMAYE KIMEELEWEKA INTER

**Afuzu vipimo, ajifunga hadi Juni 2024 huku akielezwa kuvuta euro 380,000 kwa wiki ikiwa...**

**MILAN,** Italia

CHRISTIAN Eriksen ametua Milan wakati huu akitarajiwa kujiunga na Inter Milan akitokea Tottenham.

**Nyota huyo wa kimataifa wa Denmark alitua katika ardhi hiyo juzi, Jumatatu tayari kwa vipimo vya afya kwa 'Nerazzurri' hao na kwa mujibu wa Dail Maily, tayari Eriksen, 27, amefuzu vipimo hivyo.**

Inter inatarajiwa kulipa ada ya uhamisho kiasi cha euro milioni 20 kwa nyota huyo mwenye umri wa miaka 27, ambaye mkataba wake na Spurs unamalizika mwishoni mwa msimu huu wa 2019-20.

Eriksen ameripotiwa kusaini mkataba hadi Juni 2024 ambao utakuwa unamfanya kulipwa euro 380,000 kwa wiki ikiwa ni pamoja na nyongeza.

Mustakabali wake wa baadaye umekuwa moja ya sakata lililozua mvutano katika dirisha hili la usajili, wakati Inter awali ikishindwa kukubaliana dili hilo na Spurs licha ya hatari ya Eriksen kuondoka akiwa huru mwishoni mwa msimu.

Kocha Mkuu wa Spurs, Jose Mourinho baada ya sare ya bao 1-1 kwenye Kombe la FA dhidi ya Southampton Jumamosi, alikiri kuwa hali ya mazungumzo ya muda mrefu yalikuwa yamemwacha akiwa amechanganyikiwa.

"Si makosa ya Tottenham kwamba tarehe 25 ya Januari tuweka katika hali hiyo," alisema.

"Kitu pekee ninachoweza kusema ni Eriksen, tangu alipotua, amekuwa akiheshimu kwa njia ya kitaaluma sana, na mimi na timu.

"Tottenham ni ya mwisho kulaumiwa kwa hali hii, lakini kuwa tarehe 25 ya Januari katika hali kama hii sio nzuri."

Spurs pia ilithibitisha Jumatatu kuwa Brandon Austin anajiunga na Viborg kwa mkopo hadi mwishoni mwa msimu.

Kipa huyo mwenye umri wa miaka 21, ambaye alitia saini mkataba mpya na Spurs utakaomalizika Desemba 2022, atahamia Denmark kutegemea na kibali cha kimataifa.

## ZISIKUPITE

### ARSENAL HOFU KWA AUBA

ARSENAL inatarajia kuwaona mabingwa wa Hispania, Barcelona wakimfuata mshambuliaji wao, Mgabon Pierre-Emerick Aubameyang, 30. ***(Telegraph)***

### UTD KURUDI KWA FERNANDES

MANCHESTER United inazingatia kuongeza ofa kwa kiungo wa Sporting Lisbon, Mreno Bruno Fernandes, 25, kabla ya dirisha dogo la Januari kufungwa Ijumaa wiki hii. ***(Guardian)***

### CAVANI AKARIBIA ATLETICO

ATLETICO Madrid inakaribia kufikia mazungumzo na Paris St-Germain, kuhusu uwezekano wa kumsajili mshambuliaji wa kimataifa wa Uruguay, Edinson Cavani, 32. ***(ESPN)***

### ASTON VILLA KWA STURRIDGE

ASTON Villa imetoa ofa ya pauni milioni 4.2 ya kumsajili mshambuliaji wa zamani wa Chelsea na Liverpool, Daniel Sturridge, 30, kutoka Trabzonspor. ***(Talksport)***

### CEBALLOS ANUKIA VALENCIA

REAL Madrid wanauwezekano wa kumkubalia Dani Ceballos kujiunga na miamba wenzao wa La Liga, Valencia kufuatia kiungo huyo Mhispania mwenye umri wa miaka 23, kutaka kuondoka mapema Arsenal. ***(Marca - in Spanish)***

### JESUS AMKUBALIA GUARDIOLA

MSHAMBULIAJI wa Manchester City, Mbrazil Gabriel Jesus, 22, amesema kocha Pep Guardiola alikuwa sahihi kumpokonya jukumu la kupiga penalti na akasisitiza Kipa Mbrazil Ederson, 26, anaweza kuziba nafasi yake hiyo. ***(Standard)***

### CHELSEA NAYO KWA PIATEK

CHELSEA inafuatilia hali ilivyo ya uwezekano wa kumpata mshambuliaji wa AC Milan, Krzysztof Piatek, 24, anayewindwa na Tottenham, wakati huu ikimuona kama mbadala wa Edinson Cavani, endapo watamkosa nyota huyo wa Uruguay. ***(Telegraph)***

### ARSENAL YAMPOTEZEA MARI

ARSENAL imebadili gia angani kuhusu dili la kumsajili beki wa Flamengo, Mhispania Pablo Mari, 26, kutokana na vipimo vya afya na tayari amerudi Brazil. ***(ESPN)***

### BERGWIJN NJIA NYEUPE SPURS

MSHAMBULIAJI wa Uholanzi, Steven Bergwijn, 22, amekanusha kwamba amekataa kuichezea PSV Eindhoven Jumapili huku kukiwa na mazungumzo ya kujiunga na Tottenham na inaelezwa kwamba ataruhusiwa kujiunga na klabu hiyo kabla ya dirisha hili kufungwa Ijumaa. ***(90min)***

### ARSENAL NAYO KWA EMRE CAN

MANCHESTER United, Arsenal na Tottenham zinavutiwa kumsajili kiungo Mjerumani Emre Can, 26, kutoka Juventus. ***(Metro)***

### ROSE, KYLE WA MKOPO

MABEKI wa pembeni wa Tottenham na England, Danny Rose, 29 na Kyle Walker-Peters, 22, wanatarajiwa kuondoka Spurs kwa mkopo kabla ya dirisha la usajili kufungwa Ijumaa. ***(Standard)***

HABARI MICHEZO

## Kijitonyama Veterans yapata mabosi wapya

**Na Mwandishi Wetu**

HATIMAYE timu ya Kijitonyama Veterans imepata viongozi wapya watakaoiongoza kwa kipindi cha miaka minne baada ya kufanya uchaguzi wake.

Katika uchaguzi huo uliofanyika kwenye Uwanja wa Bora, Kijitonyama jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, Mwenyekiti aliyeshinda ni Lupiana Michael 'Rashford', Makamu Mwenyekiti ni Petro Malima 'Sadio Mane'.

Wakati katibu akiwa ni Amon Petro, Mratibu Majuto Omary huku Mweka Hazina akiwa ni Ally Feruzi 'Teacher', wakati nafasi ya Ofisa Habari ikiangukia kwa Wilbert Molandi.

Pamoja na viongozi wa kuchaguliwa, wajumbe wanne waliteuliwa kuunda Kamati ya Utendaji ambao ni Talib Chuji, John Mbitu 'Morata', Hamza Nzowa na Khalid Kahatano 'Messi'.

Akizungumzia uchaguzi huo, Afisa Habari wa timu hiyo, Molandi alisema baada ya uchaguzi sasa wataelekeza nguvu katika kuijenga klabu yao ili itimize malengo yake ya kukuza mchezo wa soka.

"Baada ya uchaguzi huo, sasa hivi viongozi wote tunaelekeza nguvu katika kuifanya timu yetu inakuwa bora na yenye mafanikio na kikubwa kufikia malengo tuliyokubaliana katika kipindi hichi ambacho viongozi wapya wameingia madarakani," alisema.

## Judo waanza kujifua kuelekea Nairobi

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya Taifa ya mchezo wa Judo inaendelea kujifua kuelekea mashindano ya Afrika Mashariki, yatakayofanyika jijini Nairobi nchini Kenya kuanzia Machi 3-9, mwaka huu.

Akizungumza na Nipashe mwishoni mwa wiki, Katibu mkuu wa timu hiyo, Inocent Malya alisema kambi rasmi itaanza Februari 15 na kwamba kwa sasa kila mchezaji anafanya mazoezi binafsi akitokea nyumbani.

"Sasa hivi kila mchezaji anafanya mazoezi binafsi huku wakisubiri siku ya kuripoti kambini ifike," alisema Inocent.

Katibu huyo alisema endapo kama bajeti yao itakaa sawa, kikosi kitakachoingia kambini kitakuwa cha wachezaji 24 na ikienda ndivyo sivyo watalazimika kuondoka na baadhi yao ambapo hata hivyo kutaji idadi yake.

Alisema timu hiyo itaondoka nchini Machi Mosi, mwaka huu, ili kwenda kujiandaa na mtanange huo ambao utashirikisha timu zote za Taifa za Ukanda huu.

# KABWILI AWASHA MOTO SIMBA, TFF

**Mwandishi Wetu**

KAULI iliyotolewa na kipa wa Yanga, Ramadhani Kabwili kuwa kuna viongozi wa Simba walitaka kumhonga gari ili afanikishe mpango wa kupanga matokeo, imewasha moto katika klabu hiyo ya mtaa wa Msimbazi, Kariakoo jijini Dar es Salaam.

**Kabwili alitoa kauli hiyo wakati akizungumza na kituo kimoja cha redio nchini, ambapo alieleza kuwa Simba ilimshawishi afanye kosa kwenye mechi dhidi ya JKT Tanzania litakalomfanya aonyeshwe kadi ya njano na kufikisha idadi ya kadi zitakazomsababisha akose mechi iliyofuata baina ya watani wa jadi msimu uliopita.**

Hata hivyo, Kabwili aliyesimama langoni kwenye mechi dhidi ya Simba Februari 16, mwaka jana, Yanga ikichapwa 1-0, kwa bao pekee la mshambuliaji Mnyarwanda Meddie Kagere katika dakika ya 72, alisema hakukubali kushiriki mpango huo.

Tayari Shirikisho la Soka nchini (TFF), limeagiza Kamati yake ya Maadili kufuatilia ukweli kuhusu tuhuma hizo za upangaji matokeo zilizotolewa na Kabwili.

Taarifa ya Ofisa Habari wa TFF, Clifford Ndimbo juzi ilieleza kwamba baada ya shirikisho kusikia tuhuma hizo zilizotolewa na Kabwili kupitia vyombo vya Habari, Sekretarieti imeandikia barua Kamati yake ya Maadili kufanyia kazi suala hilo.

Aidha, TFF pia imeeleza itavijulisha vyombo vingine vya usalama ili visaidie uchunguzi na kuchukua hatua stahiki.

Hata hivyo, Klabu ya Simba jana ilionyesha kukerwa na kukasirishwa na kauli hiyo ya Kabwili, na katika taarifa yake, imeeleza: "Klabu ya Simba imepokea kwa masikitiko kauli ya mchezaji Ramadhani Kabwili aliyoitoa Januari 27, 2020.

"Kauli za aina hii kutoka kwa wachezaji ni za kuchukiza na sio za heshima ambazo zinaashiria upangaji wa matokeo ya mechi kama ilivyotuhumiwa na mchezaji huyu. Kauli ambazo Klabu ya Simba inazipinga na kukemea vikali."

Taarifa hiyo iliendelea kufafanua kuwa kauli kama hizo zina madhara makubwa kwenye uadilifu wa Klabu ya Simba na viongozi wake na kwamba uadilifu na heshima ya TFF kwa ujumla unawekwa mashakani kama kauli za namna hiyo hazitachukuliwa hatua kali.

"Klabu ya Simba inafurahishwa na hatua za haraka zilizochukuliwa na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania dhidi ya kauli kama hizi kwa vyombo husika. Klabu ya Simba inaamini kwamba jambo hili liko mbele ya mikono ya vyombo husika na litachukuliwa hatua stahiki kwa haraka," iliongeza taarifa hiyo.

Kwa upande wa Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, alisema wapo tayari kutoa ushirikiano watakaohitajika kutoa kwa TFF na vyombo husika baada ya kuzungumza na Kabwili ili kukomesha vitendo kama hivyo vinavyozuia ukuaji wa soka la Tanzania.

Lakini pia, Bumbuli alikiri Kabwili kwenda kinyume na taratibu za klabu hiyo zinazozuia wachezaji wake kwenda kuongea moja kwa moja na vyombo vya habari pasipo ridhaa ya klabu.




Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa SportPesa, Tarimba Abbas (katikati) na Mwenyekiti wa Namungo FC, Hassan Zidadu wakionyesha jezi zitakazotumiwa na klabu hiyo baada ya jana kampuni hiyo kuingia mkataba wa kuidhamini wenye thamani ya Sh. milioni 120 kwa mwaka. Kulia ni Katibu Mkuu wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), Wilfred Kidao. **NA MPIGAPICHA WETU**

## *SportPesa waimwagia mamilioni Namungo FC*

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI leo ikishuka Uwanja wa Taifa kuvaana na wenyeji wao, Simba, kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara, Klabu ya Namungo FC itakuwa na morali wa hali ya juu baada ya

Kampuni ya Kubashiri Matokeo ya SportPesa kuimwagia mamilioni ya shilingi. Namungo iliyopo nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara ikiwa na pointi 28, baada ya kushuka dimbani mara 15 msimu huu, jana imeingia mkataba wa udhamini na SportPesa wenye thamani ya Sh. milioni 120 kwa mwaka.

Akizungumza kwa niaba ya SportPesa, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa SportPesa, Tarimba Abbas alisema nia ya SportPesa imekuwa ni kuendeleza soka la Tanzania na kuongeza ushindani miongoni mwa timu za Ligi Kuu.

"Nadhani mnakumbuka siku zote tumekuwa tukisema SportPesa imekuja Tanzania kwa nia ya kuendeleza sekta ya mpira wa miguu, ndio maana tuliingia mikataba na klabu kubwa Tanzania kama Simba, Yanga na Singida United. Pia tulitoa sapoti ya kifedha na vifaa vikiwamo jezi kwa timu ya Polisi Tanzania, vitu ambavyo vimekuwa chachu kwa wao kuingia Ligi Kuu," alisema Tarimba.

Aliongeza kuwa wanaimani kubwa na Namungo FC ambayo ipo nafasi ya tano kwenye Ligi Kuu na ndiyo maana wameamua kuweka udhamini huo wakiamini wanaweza kufanya vizuri na kutoa upinzani msimu huu na ujao.

Kwa upande wa Namungo FC, Mwenyekiti wa timu hiyo, Hassan Zidadu aliwashukuru SportPesa kwa udhamini huo na kuahidi kutumia fursa hiyo vizuri kutimiza malengo ya wadhamini hao.

"Tunawashukuru sana SportPesa kwa kutupa fursa hii kwa timu yetu na tunatoa ahadi ya kufanya vema ili tuchukue ubingwa wa Ligi Kuu au Kombe la Shirikisho ili tuweze kuitangaza chapa ya SportPesa kimataifa," Zidadu alisema.

"Hili ni jambo la furaha kwa timu yetu kuweza kupata udhamini wa kampuni kubwa kama SportPesa, hakuna asiyefahamu ukubwa wa kampuni hiyo ambayo ipo kwenye udhamini na klabu mbili kubwa Tanzania, Simba na Yanga. Lakini pia ni wadhamini wakuu wa klabu kubwa Uingereza Everton. Kwahiyo tunafurahi kuwa sehemu ya familia ya SportPesa."

# Michezo

Jumatano Januari 29, 2020

Nipashe





Eriksen hatimaye kimeeleweka Inter UKURASA 30




Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Klabu ya Simba, Mohamed 'Mo' Dewji, akimkabidhi jezi ya klabu hiyo, Rais wa Shirikisho la Soka Duniani (Fifa), Gianni Infantino, baada ya kufanya mazungumzo naye makao makuu ya shirikisho hilo, Zurich, Uswisi jana. **PICHA: MTANDAO**

## Ulimwengu arudi kujiuliza TP Mazembe

**Na Mwandishi Wetu**

HUKU Mbwana Samatta jana akianza kuichezea klabu yake mpya ya Aston Villa dhidi ya Leicester City kwenye Kombe la Ligi England, mshambuliaji Mtanzania mwenzake waliyeng'ara naye TP Mazembe amerejea kuitumikia klabu hiyo ya DR Congo.

Samatta na Ulimwengu waliipaisha Mazembe wakati wakiitumikia kwa pamoja kabla ya wawili hao kuondoka mwaka mmoja na nyota huyo wa sasa wa Aston Villa kujiunga na KRC Genk ya Ubelgiji. Klabu hiyo ya DR Congo kupitia mtandao wake wa Instagram jana ilitangaza: Klabu ya TP Mazembe ina furaha kutangaza kurudi katika safu ya wachezaji wake, Thomas Ulimwengu. Winga huyo wa kimataifa wa Tanzania ametia saini mkataba wa miaka miwili.

"Akiwa na umri wa miaka 27, Ulimwengu anarudi katika dimba la Kamalondo ambako aliondoka mwaka 2018. Winga huyo wa Kitanzania anarudi akitoka kusaka nafasi ya kucheza Ulaya, hali iliyomsumbua kwani uwezo anao ila hakuwa na bahati."

# MO AIPELEKA SIMBA FIFA IKIIVAA NAMUNGO

## Huko England Salim Kikeke naye amuita Ferdinand Msimbazi, huku Dar kukinukisha usiku...

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Simba ikitarajiwa kushuka dimba la Taifa leo saa moja usiku kuikaribisha Namungo FC kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya klabu hiyo, Mohamed 'Mo' Dewji, amekutana na kufanya mazungumzo na Rais wa Shirikisho la Soka Duniani (Fifa), Gianni Infantino, katika makao makuu ya shirikisho hilo, Zurich, Uswisi.

**Katika mazungumzo yao, wawili hao waligusia mipango ya Fifa kuendeleza soka barani Afrika, Dewji akieleza matumaini yake juu ya maendeleo ya mpira wa miguu barani katika uongozi wa Infantino.**

"Kwa kweli, nimefurahishwa sana kwa dira na shauku ya kuendeleza mpira wa ushindani na shauku Afrika. Nia ya Fifa ni kuboresha maendeleo ya mpira.

"Najua chini ya uongozi wa Gianni, mpira wa miguu kwenye bara letu, utaenda 'next level' (utapiga hatua zaidi)," Dewji alieleza baada ya mazungumzo yake na bosi huyo wa Fifa.

Aidha, Dewji alimkabidhi Infantino jezi ya Simba ikiwa imeandikwa jina la rais huyo ambaye amekuwa mstari wa mbele katika kupiga vita rushwa michezoni na ufujaji wa fedha uliokuwa ukifanywa ndani na nje ya shirikisho hilo kwa wanachama wake.

Dewji, mmoja wa mabilionea vijana barani Afrika, ameifanya Simba kuwa miongoni mwa klabu zinazoendeshwa kwa kisasa Afrika na sasa inatajwa kama timu inayotarajiwa kuwa tishio ndani ya miaka michache ijayo barani Afrika.

Katika hatua nyingine Balozi wa Simba jijini London, Salim Kikeke jana alikutana na Mkurugenzi wa Mpira wa Miguu wa QPR, Les Ferdinand na Mkurugenzi wa Ufundi ambaye amewahi kuwa kocha wa timu hiyo, Chris Ramsey kujadili namna klabu hiyo itashirikiana na Simba katika maendeleo ya soka la vijana.

Hatua ambayo Klabu ya Simba imeelezea kuwa "mambo makubwa yanakuja hivi karibuni."

Simba ambayo inaongoza msimamo wa Ligi Kuu Bara ikiwa na pointi 41, baada ya kushuka dimbani mara 16 msimu huu, leo itaanza raundi ya pili ya ligi hiyo kwa kuikaribisha Namungo FC ya mkoani Lindi.

Simba itashuka dimbani ikitoka kuichapa Mwadui FC mabao 2-1 kwenye mechi ya Kombe la FA, wakati Namungo iliyopo nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi Kuu baada ya kucheza mechi 15 za raundi ya kwanza, nayo ikipata ushindi kama huo dhidi ya Biashara United katika michuano hiyo ambayo bingwa huiwakilisha nchi kwenye Kombe la Shirikisho Afrika.

Hata hivyo, kuelekea mechi hiyo wakati uongozi wa Namungo ukieleza wanatambua Simba ni timu kubwa na wanaiheshimu, Kocha Mkuu wa 'Wekundu wa Msimbazi' hao, Mbelgiji Sven Vandenbroeck amesema tayari ameshabaini licha ya kwamba wapo kileleni mwa msimamo wa ligi, lakini hakuna timu ndogo na amebaini ugumu anapokutana na timu hizo.

Sven ambaye ameiongoza Simba kwenye mechi sita za ligi dhidi ya Lipuli FC, KMC, Ndanda, Yanga, Mbao na Alliance FC na kudondosha alama mbili tu kati ya 18 alizopaswa kuzivuna, amesema ugumu wa ratiba pamoja na changamoto kali wanayokutana nayo wanapocheza na wapinzani wao, umempa mbinu mpya ya kuweza kuzikabili.

"Wakati nakuja hapa nchini nilifikiri kila kitu kitakuwa rahisi tu, lakini nimegundua ni tofauti kabisa, ligi hii ni ngumu na timu zote zinapambana," alisema.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >